JULAI MMXXV - TOLEO LA XLV

# NGURUMO
## *ya Mwandishi*




**HABARI KUU:**

**Dirisha la Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu Msimu wa Nne Lafunguliwa**

## YALIYOMO

**TAHARIRI— Uk 02**
'SIYO LAZIMA'

**MWANDISHI WETU— Uk 03**
SALUM SAID NGUATE

**NEW IN TOWN: Uk 04**
MJUE BINADAMU NA MENO YA MBWA

**PITIO LA VITABU— Uk 05**
KILIO CHETU '4'

**SAIKOLOJIA: Uk 06— 07**
UHUSIANO KATI YA UPENDO NA TOFAUTI YA UMRI

**MAKALA: Uk 08 - 09**
UANDISHI WA RIWAYA NA HATUA ZAKE

**KUTOKA KWA FANANI: Uk 10**
SALUM MAKAMBA ATUFUNZA

**SAKO KWA BAKO – Uk 11**
FUNDI MITINDO ANAYEVIJUA VITABU

**RIWAYA: Uk 12—13**
MSALITI '6'

**RIWAYA: Uk 14—15**
Najutia Kuwa Na Wewe '6'

**YA KALE NI DHAHABU: Uk 16**
Alibaba na Wezi 40 '21'

**HABARI MOTO: Uk 17**
TUZO YA TAIFA YA MWALIMU NYERERE

**SHUBAKA LA VITABU: Uk 18**
HISTORIA YA VITABU 'THE EGYPTIAN BOOK OF DEATH'

**KITABU NILICHOSOMA: Uk 19**
THE HAPPIEST MAN ON EARTH

**MATANGAZO: Uk 20**

**MALENGA WA KILEO: Uk 21**
NIMEMISS PISHILE

**HABARI PICHA: Uk 22**

**KUTOKA MAKTABA: Uk 23**
Maisha ni Mapambano '11'

**ELIMU JAMII: Uk 24 & 25**
SAFARI YA MALEZI— MALEZI YA KUEPUKA

**HADITHI: Uk 26 - 27**
Happy New Year '8'

**HADITHI: Uk 28 - 29**
NGUVU YA KIAPO '03'

## TAHARIRI:
# SIYO LAZIMA...

Salaam kwenu ndugu zangu,
Natumai mu wazima bukheri wa afya, nami pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa hili.

Karibuni tena katika toleo letu hili la 45 linalotuambia 'SIYO LAZIMA'. Hakika, siyo lazima kufanya hilo unalolifikiria kwa sasa. Katika maisha hapa duniani, hususan sisi vijana tuna ndoto na maono mengi sana ya kuijenga kesho yetu. Ni jambo zuri mno maana asiye na maono au ndoto za kesho yake ni marehemu pekee.

Leo hii tunashuhudia vijana wengi wakijiingiza kwenye mambo ya hatari kwa maisha yao au yanayovunja heshima yao kwa jamii ili tu wapate kuijenga kesho yao. Sawa! Lakini hilo ambalo unataka kulifanya, kabla ya kulifanya umejiuliza kama ni lazima au siyo lazima kulifanya? Kwamba nisipolifanya nitapata hasara gani?

Katika utafutaji wetu, yatupasa kuweka mezani yale ya 'Lazima' kufanya na yale ambayo 'Siyo ya Lazima'. Kwanini siyo ya lazima? Siyo ya lazima kwa sababu labda nikifanya nitahatarisha afya na uhai wangu, au jamii itanitazamaje, nitaendana na imani yangu ya kidini?

Tunapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kuijenga kesho yetu. Ndiyo! Lakini siyo lazima niutweze utu wangu kwa ajili ya hilo, siyo lazima nihatarishe maisha yangu kwa ajili ya hilo, siyo lazima niwe mshirikina kwa ajili ya hilo.

Kwahivo neno 'Siyo Lazima' twapaswa kuliishi katika maisha yetu ili kutujengea roho ya kiasi katika maamuzi.

Asante!

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

# MWANDISHI WETU:
## SALUM SAID NGUATE

**Katika toleo letu la 45, kupitia safu hii ya MWANDISHI WETU tunamleta kwenu Salum Nguate. Wengi, wale wapenzi wa hadithi mitandaoni, jina hili siyo geni kabisa.**

**Basi yeye ni nani? Na safari yake kiuandishi ilianzia wapi?**

Jina langu ni SALUM SAID NGUATE, nimezaliwa tarehe 20 Agosti 1993 Kijiji cha Chingulungulu kata ya Muhuwesi wilaya ya TUNDURU mkoani Ruvuma

Mimi ni mtoto wa tano kati ya watoto sita wa baba yangu na mama YANGU

Nilianza elimu ya msingi mwaka 2002 na kuhitimu mwaka 2008 katika shule ya msingi Ngatuni hapo hapo kijijini kwetu.

Mwaka 2009 nilianza elimu yangu ya sekondari Shule ya Secondary NANDEMBO huko huko wilayani TUNDURU ila nilishindwa kuendelea na shule baada ya baba yangu kufariki 2010. Huo ndiyo ukawa mwisho wangu wa kuendelea na masomo

Kifupi nimeishia form 2

Baada ya mihangaiko mingi na ujanja wa *yes-no*, 2012 niliamua kuja mjini na kujifunza kuchomelea mageti, ndo kazi yangu Hadi Sasa inipayo riziki na kunifanya niishi

Kipaji au *hobby* ya uandishi wa riwaya na SIMULIZI ilianza tangu nikiwa shule ya msingi. Nilikua napenda sana kuandika na kusoma hivyo niliandika riwaya nyingi sana na hadithi hadi wakaanza kuniita jina la Shigongo

Kwanza napenda sana kusoma na kutunga na nilianza tangu shule kwa kuandika story za kufurahisha marafiki. Ukiachana na uandishi mimi ni fundi kuchomelea mageti madirisha vitanda meza milango viti n.k yaani *welding.*

Mpaka Sasa nimeandika hadithi tatu

1-TEARS IN MY HEART

2-MAKOSA 35 YA MAISHA YANGU

3-SALHA

Najitahidi sana kuandika lakini kuna muda tunakatishwa tamaa na watu wachache wasiopenda taaluma yetu mfano unatumia muda mwingi kuandika mtu anakuja anakopi na kutuma kwenye kurasa zake.

Lakini pamoja na yote hayo ndoto yangu nahitaji Dunia inijue na kunifahamu kupitia tasnia hii nahitaji niwe mwandishi mkubwa kama RICHARD MWAMBE, ERICK SHIGONGO, E.A MUSIBA na wengineo. Niwe mwandishi wa makala na riwaya mbalimbali.

Kiukweli waandishi wanaonivutia sana na ninaowafuatilia kazi zao ni Richard mwambe na Hayati E.A MUSIBA

Neno langu kwa waandishi hawa ni kwamba wasichoke kutuunga mkono waandishi chipukizi, waamini katika sanaa yetu waamini katika tufanyacho

Mtu yeyote akitaka kusoma kazi zangu atanipata kwenye WhatsApp channel ya

JUMBA LA SIMULIZI



**SALUM SAID NGUATE**

Na namba zangu za simu ni

**0784989666**

Facebook page ni

**Story za Nguate**

Instagram ni

**salum nguate**

Twitter 'X' ni

**snguate**

WhatsApp

**0784989666**

Email: **salumnguate9@gmail.com**

Asanteni na karibuni mnisome.

# NEW IN TOWN :

## Mjue Binadamu... na Meno ya Mbwa

**MJUE BINADAMU NA NGUVU ZILIZOMO NDANI YAKE**

**Mwandishi: Chelestino Malinga**

Kabla ya mwanadamu kuuliza dunia ni nini, alipaswa ajiulize: "Mimi ni nani?" Kitabu hiki si cha kujibu tu, bali cha kufungua mlango wa ndani - mlango ambao wengi huupita wakizani ni ukuta.


Ndani ya kurasa hizi, msomaji atasafiri kwa miguu ya fahamu, kupitia misitu ya asili, upepo wa ndoto na milima ya tahajudi. Atakutana na ukweli wa nguvu zilizopo ndani ya mwili na zile zinazozunguka nje ya mipaka ya macho. Kutoka kwa uhalisia wa maumbile hadi ushawishi wa nguvu ya kujamiiana, kutoka kivuli cha uchawi hadi mwanga wa kiutambuzi - haya ni mafumbo ambayo hayahitaji kuaminiwa, bali kuamshwa ndani ya nafsi yako mwenyewe.

Hii si ya kusomwa kwa haraka - ni mwaliko wa kunyamaza na kusikiliza kilicho ndani yako.

**Kitabu hiki kinapatikana kwa Tsh 15,000:**
**Dar es salaam duka la Kona ya Riwaya Kinondoni: 0655428085**
**Au kwa kumpigia simu mwandishi 0754062900/0655062900**




**MENO YA MBWA**
**Mwandishi: KALMAS KONZO**




Veneranda anakumbana na maisha ya uyatima angali yu mtoto mdogo sana. Ulimwengu unamtenga na kuyafanya maisha yake kutokuwa rahisi chini ya ulezi wa mama yake wa kambo.

Alipitia magumu mengi yenye kukatisha tamaa ya maisha. Taabu na mateso ya kila aina viliandamana kwake kila uchao.

Je nini hatima ya Veneranda?

**Kitabu hiki kinapatikana kwa Tsh 10,000:**
- **Dar es salaam duka la Kona ya Riwaya Kinondoni 0655428085**
- **Dar es salaam Posta Mpya kwa George 0755454152**
- **Kalmas Konzo - 0625646265**




*Inaendelea...*

iv. Nafasi ya mwanamke katika jamii

Nafasi ya mwanamke ni jumla ya mambo yote ayatendayo mwanamke katika kazi ya fasihi. Mengine huwa mazuri yanayostahili pongezi na machache huwa mabaya yanayostahili kukemewa kwa nguvu. Katika tamthiliya hii, mwanamke amechorwa kama;

- Chombo cha starehe. Mfano Joti anamtumia Suzi kwa ajili ya kujistarehesha.

- Asiyependa mabadiliko. Mama Suzi hataki kutoa elimu ya jinsia kwa wanaye.

- Asiye na maadili. Suzi hana maadili, anajiingiza katika mahusiano ya kimapenzi katika umri mdogo.

- Mwenye elimu na asiyedanganyika. Anna ana elimu ya jinsia na mahusiano, wanaume wanashindwa kumdanganya kwa pesa na maneno matamu.

**UJUMBE**

i. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu. Suzi na Joti hawakufunzwa vyema na wazazi wao, badala yake ulimwengu unawafunza.

ii. Elimu ya jinsia na mahusiano itolewe kwa watoto. Elimu hii itawafanya waepuke vishawishi.

iii. Sheria kali zitungwe dhidi ya watu wanaowalaghai watoto. Kuna watu wazima wanaowaingiza watoto katika vitendo vya kimapenzi kama Chausiku anavyomlaghai Joti. Sheria kali itungwe na isimamiwe kuwakomesha.

iv. Wazazi wote washirikiane katika malezi ya watoto. Baba Anna na Mama Anna wanashirikiana katika malezi ya watoto wao. Matokeo bora yanaonekana.

**MIGOGORO**

Migogoro iliyojitokeza ni pamoja na;

Migogoro ya wahusika

i. Mgogoro wa Joti na Suzi

Mgogoro huu unasababishwa na tabia ya joti kuwa na mahusiano na wasichana wengi. Suluhisho la mgogoro huu ni Joti kumuomba msamaha Suzi.

ii. Mgogoro wa Suzi na Mama yake

Mgogoro huu unasababishwa na mama Suzi kuvikuta vidonge vya kuzuia mimba katika sketi ya mwanaye. Suluhisho la mgogoro huu ni Mjomba kumwamuru Suzi aende ndani na mazungumzo kati ya Mjomba, Mama Suzi na majirani wengine yanaendelea.

iii. Mgogoro kati ya Mjomba na Mama Suzi

Chanzo cha mgogoro huu ni Mjomba kumshauri Mama Suzi ampe elimu ya jinsia na mahusiano binti yake. Mama Suzi anakataa na kusema kufanya hivyo ni kuwafundisha watoto umalaya.

iv. Mgogoro kati ya Chausiku na Joti

Chausiku anamlaumu Joti kuwa anamahusiano na wasichana wengine, anaendelea kulalama kuwa, hata zawadi anazompatia anawapatia wasichana wengine. Chausiku anamtisha Joti kuwa atamchoma moto yeye na visichana vyake. KICHEKO!!

Mgogoro wa nafsi

Huu ni mgogoro ambao humpata mhusika peke yake kati yake yeye na nafsi yake.

- Suzi anapatwa na mgogoro wa nafsi pale anapopata mimba na kuambukizwa virusi vya UKIMWI.

***Itaendelea..***

SOMA VITABU
- Kwa afya ya ubongo wako
- Kwa kujiongezea maarifa
- Kwa burudani

USISITE
- Kumsimulia mwingine hadithi uliyosoma
- Kumfundisha mwingine yale uliyojifunza
- Kumshauri mwingine kitabu cha kusoma

NI VIZURI
- Kutembelea maktaba
- Maduka ya vitabu
- Kupiga stori na waandishi

# UHUSIANO KATI YA UPENDO NA TOFAUTI YA UMRI



## UHUSIANO ULIOPO KATI YA UPENDO NA TOFAUTI YA MIAKA.

Mungu ni mwema hata tumekutana tena katika toleo hili la jarida la NGURUMO YA MWANDISHI. Hongera kwa kuuvuka mwezi 6 na 7 hata sasa tumeshaingia mwezi wa 8. Kwa yale ambayo hayakufanikiwa kwa mwezi au miezi iliyopita, tamkia ushindi na kisha shinda kutokana na juhudi zako na kudra za Mungu baada ya kumuomba kila itakiwazvyo.

Leo kwenye Makala ya kisaikolojia, tuangazie swala zima la mahusiano katika nafasi muhimu ya umri.

Kila binadamu na wakati wake wa kuzaliwa na wakati wa kufa. Ni mara chache sana na pengine imetokea mara mbili au tatu kuwa wanandoa wameoana wote walizaliwa siku moja. Ni kawaida sana kukuta watu walio kwenye mahusiano au ndoa wakawa wamepishana umri. Mara nyingi sana utakuta mwanaume amemzidi umri mwanamke, mara chache sana utakuta mwanamke ndie mkubwa kwa mwanaume, mara chache zaidi utakuta wapenzi wanalingana.

Mapenzi ni hisia na upendo wa kweli, popote yanaweza kuonekana, iwe mwanaume kumzidi umri mwanamke au mwanamke kumzidi umri mwanaume ilimradi upendo wa kweli upo basi mara nyingi suala la umri hasa mwanaume kumzidi mwanamke haijawahi kuwa ajabu, ila mwanamke kumzidi mwanaume umri bado jamii haijazoea.

Tafiti nyingi za wataalamu wengi zimempa mwanamke nafasi kubwa sana ya kuwa ni kiumbe chenye nguvu zaidi ya mwanaume. Inaaminika kuwa, mwanamke anaufahamu na nguvu ya ndani mara kumi Zaidi ya mwanaume. Tafiti nyingi zimempa mwanamke umri mara kumi zaidi ya mwanaume kulingana na utashi na uwezo wa kuhimili jambo. Yaani hapo mlipo, hiyo miaka aliyonayo mkeo au mpenzi wako, muongezee na miaka kumi zaidi, hivyo ikiwa mkeo ana miaka arobaini na mbili [42] basi muongezee miaka mingine 10 ili awe na miaka hamsini na mbili [52]. Akili ya mwanamke ina uwezo mkubwa sana wa kuchanganua na kuhimili mambo kuliko mwanaume. Hiyo ni asili ya uumbaji tangu kuumbwa kwa ulimwengu na ndio maana hata biblia inasema “Mwanaume ishi na mwanamke kwa akili”.

Ikiwa mahusiano ya mwanamke na mwanaume yakatengewa chumba maalum na kuchunguzwa hatua zao, utashangazwa sana na mambo yao. Ikiwa wapendanao wakafatiliwa kutokana na yale wayatendayo ni wazi kuwa mengine yatafurahisha na mengine yatakuacha mdomo wazi kutokana na uajabu wake.

Mapenzi ni matamu na ni mazuri sana, ila ikiwa mtaelewana na kuendana na kuchukuliana hisia zenu husika. Ikiwa mwanamke ana miaka 30, mwanaume ana miaka 35, kitaalamu hapo mwanamke ni mkubwa, mwanamke atakua na miaka 40 huku mwanaume akiwa na miaka 35, watu hao ni lazima mawasiliano na maisha yao yawe ni kugombana na kupatana kwa hapa na pale. Sio ajabu.

Pamoja na kuwa mwanamke ni kiumbe mwenye nguvu zaidi ya mwanaume lakini pia mwanamke ni dhaifu sana kwa mwanaume hasa akimpenda. Mwanamke akipenda, hata awe mkubwa kiasi gani, akipenda huwa zaidi ya mtoto. Moyo wa mwanamke pale anapopenda huweza kufanya mambo makubwa kulingana na moyo wake unavyomtuma. Kisaikolojia, mwanamke anapopenda uwezo wake wa kufikiri juu

ya mpenzi wake huwa ni mdogo sana, huwa chini ya 10%, ni mpaka pale anapohisi au anapotendwa ndio akili humrudia na kugeuka kuwa zaidi ya jasiri katika mahusiano hayo.

**KIPI NI BORA, MWANAMKE AWE MDOGO AU MMWANAUME AWE MDOGO?**

Ukiniuliza swali hilo, nitataka nikurudishe kwenye upendo wa kweli.

Upendo wa kweli haupo kwenye tofauti ya umri, ingawa jambo la kuzingatia ni kuutunza upendo wa kweli unapokutana na mpenzi wa maisha yako. Ingawa ni ukweli ulio wazi kuwa mwanamke akiwa mdogo kwa mwanaume anapata faida nyingi mfano, nafasi ya kudekezwa, nafasi ya kupendwa, nafasi ya kusikilizwa na nafasi ya kuhudumiwa kwa kipaumbele zaidi. Ni ukweli ulio wazi kuwa mwanaume anataka kutawala na kuheshimiwa, ikiwa atakua kwenye mahusiano na mwanamke aliemzidi umri ni wazi kuwa nafasi ya utawala haitokuwepo, kila atakachofanyiwa ataona kuwa anadharauliwa kutokana na udogo wake.

**NINI HUTOKEA KWENYE MAHUSIANO YA WATU WANAOLINGANA UMRI?**

Kwa kuangalia namna nilivyochambua uhalisia wa nguvu za mwanamke hapo juu, kwamba ikiwa mwanamke ana umri wa miaka 40 na mwa naume akawa na miaka 45, hapo hesabia kuwa mwanamke ana miaka 50 huku mwanaume ana miaka 45. Kwa kuzingatia hivyo ikiwa wapenzi wote wakawa na miaka 30 hapo hakuna mapenzi, na kiuhalisia ni kuwa mwanamke atakua na miaka 40. Hivyo mahusiano ya wapenzi hawa bado hayatokua na utulivu kwani kitaalamu hapo mwanamke ni mkubwa. Inaaminika mahusiano ya watu waliolingana umri ni mazuri, wengi wanawapa nafasi watu hawa kuwa ndio kwenye mapenzi ya kweli, haya ni mawazo ya wengi ila kiuhalisia kundi hili pia laweza kukumbwa na migogoro ya hapa na pale hasa pale ambapo mwanamke akitendwa. Kabla ya kutendwa mwanamke huwa sawa.

Kwa toleo hili tuishie hapa, tutaendelea wakati mwingine ili kuona faida na hasara za mahusiano ya watu wanaolingana umri.

Karibu upate vitabu vya Kisaikolojia.

**JITIBIE KISAIKOLOJIA — 15,000.**

**SAIKOLOJIA YA MAHUSIANO NA NDOA— 10,000.**

Karibu pia kupata huduma za ushauri wa kisaikolojia kuhusiana na mahusiano,mapenzi, ndoa, malezi ya watoto na vijana na maisha kwa ujumla. Huduma zote hizo wasiliana nami kupitia +255 763 013 206.

KARIBU.

The Magic Author,

Queen of psychology.

Madame Neema Mgao.

Dodoma.

Tanzania.

**KUTOKA KWA FANANI**

**USHAIRI NI BAHARI SI KIJITO**

Katika ukurasa wa 55 na 56 Prof. Mulokozi na Prof. Kahigi wanasema, "Miundo ya mashairi ni mingi kama walivyo

washairi wenyewe. Kinachofanyika mara nyingi ni kuorodhesha na kuelezea baadhi ya miundo ambayo inatumika zaidi kwenye zama na mahali fulani."

Na ndicho alichokifanya hata Prof. Nabhany katika maelezo yake. Alisema wazi kuwa kanuni alizozitamka yalikuwa ni makubaliano ya watunzi wa Lamu, Pate, Siu na baadhi ya sehemu za Mombasa. Kwa hiyo alikuwa sahihi kabisa.

Ajabu ni watu kubeba kanuni hizo kichwakichwa kisha kwa uchache wao wa elimu kuanza kulazimisha watu kuwa ndizo zinazopaswa kufuatwa na kila mtunzi. Na anayekwenda kinyume nazo ati anaunajisi ushairi na inapaswa achapwe bakora. Bila kufahamu masikini kuwa kumbe wao ndiyo wana Uhaba wa Elimu ya Ushairi Kichwani (UEUKI).

## Uandishi wa riwaya na hatua zake faafu

Na: Shabban Mngazija (kutoka mtandaoni)

UANDISHI wa Riwaya ni fani ya usanii kama fani zingine za uandishi kama vile Uandishi wa Habari, Uandishi wa Vitabu vya Taaluma, Uandishi wa Majarida, Uandishi wa Sinema, nakadhalika.

Uandishi wa riwaya unazo taratibu na kanuni zake ambazo mwandishi anapozifuata ataweza kuandika hadithi za kuvutia, zenye mafunzo na hata kuweza kuzikamilisha katika muda mfupi pasi na kuathiri shughuli zake; kwamba, kuweza kwake huko si lazima awe amekwenda chuo cha uandishi, ila kuwa na elimu ni msaada zaidi katika kurahisisha mambo kwa tafsiri ya kukuweka katika upeo mpana wa uoni. Hatahivyo, pamoja na kutokwenda chuo kwa mwandishi, bado anapaswa kujua kanuni za uandishi husika ili kuwa mwandishi bora.

**KWANINI MTU HUANDIKA HADITHI?**

Mosi – mtu huandika ili kutoa hisia zake juu ya jambo au tukio fulani kwa jamii pasi na kutarajia malipo.
Pili – mtu huandika ili kuendeleza utamaduni au simulizi za waandishi waliopita.
Tatu – mtu huandika kama sehemu yake ya maisha katika kujipatia kipato.
Nne – mtu huandika kwa sababu za kitaaluma au kama mtihani.

**HATUA ZA KUFUATA**

1. Chagua somo
2. Jiulize: je, nina utaalam wa somo hilo? Kama sina – je, nipo tayari kujifunza ili kutekeleza azma yangu?
3. Kumbuka kuwa, kuandika ni pamoja na kuelewa nini unataka kuandika.
4. Chagua mwanzo.
5.Chagua mwisho- Kwa kuchagua mwanzo na mwisho, mwandishi anapata dira ya mwelekeo wa hadithi badala ya 'kuogelea kwenye bahari ya matukio mengi' huku mengine yakiwa hayahusiani na hadithi.

6. Hapa katikati chagua mgongano wa mawazo, Ndiyo/Hapana, Furaha/Huzuni, Amani/Ugomvi, Dini/Ukafiri, Chama kimoja/Vingi, Ukuwadi/Uungwana, nakadhalika. Pendekeza mahali ambapo hadithi itahusishwa – Mjini?/Kijjini?, Tanzania?/Kwingineko?, Mchanganyiko?

7. Chagua wawakilishi wakuu na uwape majina na sifa (Elimu, sura, tabia, n.k.): mhusika mkuu (nyota) atakayekuwa toka mwanzo hadi mwisho; mhusika wa akiba kama hutaki mhusika mkuu afike mwisho; mhusika mkuu mkinzani atakayekuwa mwanzo hadi mwisho; mkinzani wa akiba kama hutaki mkinzani mkuu afike mwisho. Tengeneza fremu ya hadithi: mfano, sura ya 1, 2, 3, 4…na sura ya mwisho; hitimisha kulingana na mgongano wa mawazo uliojitokeza hadithini.

**Jinsi ya Kuandika Riwaya/ Hadithi**

Andika kwa undani sura mojamoja – fanya utafiti kwa kila tukio unalotaka kuandika ili uwe na hadithi ya kuaminika au inayoonekana ya kuaminika hata kama ni riwaya.

Ondoa mawazo potovu: kumbuka mwandishi ni kioo cha jamii – maandishi yako yanakuwa fundisho kwa wengine, ukiandika ya kupotosha jamii itapotoka, kwa maana kalamu ni kali kuliko upanga maana unaweza kulaumiwa kama sio kujikuta ukilaaniwa!

8. Piga chapa/taipu muswada ghafi – ni vyema kwa kutumia kompyuta katika zama hizi za tekinolojia ya elektroniki.

9. Chapa (print); soma na kufanya masahihisho ya awali.

10. Rekebisha makosa.
Inapendekezwa sana kufanya masahihisho mwenyewe kama unajua kutumia kompyuta kwakuwa ni rahisi kuongeza/ kuondoa mawazo na kuharakisha kukamilika kwa muswada *(tuwasifu waandishi wa zamani ambao walifanya yote kwa mkono zaidi)*

Wakati wa kufanya masahihisho, usiishie kusahihisha makosa tu, bali 'uisikilize' hadithi na kupata mantiki. Ukipata wazo jipya na bora zaidi usisite kuliweka.
Fanya hivi sura moja hadi nyingine huku ukihakikisha kila sura inajitegemea katika kupeleka ujumbe wake *(usirudie jambo lililokwishazungumziwa nyuma)*
Angalia: je, lengo lako la kumalizia limebakia kama mwanzo au mawazo mapya yamelibadilisha? Kama limebadilika kulingana na taarifa mpya, kubali mabadiliko kwani riwaya siyo msahafu! Angalia upya jina la kitabu: je, linaendana na riwaya pamoja na

umaliziaji? Kama halilingani, chagua lingine maramoja!
11. Chapa tena. Soma muswada wote na kufanya masahihisho kwa mkono.
12. Yahawilishe masahihisho ya mkono kwenye mashine. Hatua hii pia inashauriwa kuifanya mwenyewe badala ya kumpatia mpiga chapa kwakuwa inakusaidia 'kufinyanga maandishi mweyewe' pindi ukipata kosa au kujiwa na wazo jipya.

Tangu mwanzo hakikisha unatunza kazi yako isipotee. Weka nakala katika 'cd' zaidi ya moja mbali na ile ya kompyuta yako. Ikiwezekana azima nafasi kwenye kompyuta ya mwenzio kujikinga iwapo yako itaharibika na taarifa zote kupotea. Usitupe kazi yako ya mwanzo kwakuwa inayo nafasi kubwa ya kuja kukusaidia pindi ukipotea njia.
13. Chapa tena.
14. Hii ni hatua muhimu sana kuliko zote: Soma hadithi yote KAMA VILE NI YA MTU MWINGINE: Hapa unakuwa mhariri mwenyewe. Kosoa bila huruma na kutoa maoni kwa madhumuni ya kuiboresha. Jifanye wewe ndiye msomaji: kumbuka kwamba Mambo anayopenda mwandishi si lazima msomaji ayapende. Kwa kujifanya msomaji tofauti na mwandishi utaweza kugundua kasoro ndani ya hadithi. Katika hatua hii, ni vyema ukaipitia hadithi baada ya muda mrefu tangu uikamilishe; kwani kwa kufanya hivyo katika kuipatia muda, ndivyo unaipatia muda akili yako *(wakati huo utakuwa umepoa)* kuondokana na kujipendelea kwakuwa hakukusaidii katika uandishi.

Fanya utafiti wa ziada unapokuwa na wasiwasi.
Rekebisha makosa kwa mara ya mwisho. Angalia mantiki, miundo ya sentensi, misemo, nakadhalika.
15. Mpatie mtaalam kazi ya kuupitia muswada kikamilifu ikiwa ni pamoja na kurekebisha muundo na mantiki. Huyu ni mtu muhimu sana kwakuwa anakuwa kama msaidizi wako huku ukitambua kuwa si lazima ukubaliane na mawazo yake hata kama jambo moja linabakia kuwa bayana kwamba hadithi ni yako tu *(hapa nasisitiza, usikubali itekwe nyara na mwingine maana si yake ingawaje hoja inashika kwamba mara nyingi anayokueleza huwa ndiyo sahihi kuliko hata ufikiri wako, hivyo usiwe mgumu kubadilika! Ila hatushauri ukubali kuburuzwa, mwandishi mbishi ni mzuri zaidi, lakini mwandishi aambiliki ni rahisi zaidi kuburuzwa na upumbavu wake)*

Ndio, mtaalamu huyu ni mkatishaji tamaa maana hana simile katika kudhihirisha kile anachokiona si sahihi au ni utumbo! Huyu ni mfyekaji kila mahali, anaweza kufyeka asibakishe kitu katika huko kuandika kwako maana anaweza kuuchafua muswada kiasi cha kukufanya hata ushindwe kujiamini na kujiona pengine umevamia fani!

Yupo mtu mwingine unayepaswa pia kumpatia kazi yako; hatahivyo huyu si kama huyo wa awali ambaye ni 'katili', huyu ni wa kukupatia maoni tu. Mara nyingi huyu ni mkosoaji tu wala hakusaidii sana kuandika hadithi yako maana yeye huifanya kazi yake akidhani wewe unazijua kanuni kiasi akigundua kosa au makosa anaweza kushangaa ni kwa nini ufanye makosa ya kimsingi! Huyu hufikiri hadithi yako imekamilika kumbe mara nyingi sivyo.
Hivyo ni jitihada zako tu za kumuelewa anachotaka ndizo zitakazokufanya kutekeleza yale anayokuagiza; huyu kwa tafsiri nyingine ni mwalimu wako ukiwa kazini, ndiye atakayeifanya hadithi yako iwe 'hadithi' maana likitajwa jina lake *(mtu huyu anaipenda sana lugha iliyonyooka)* katika walioupitia muswada wako una uhakika wasomaji watakikimbilia kitabu chako mara kitakapokuwa kimechapishwa na kuwekwa sokoni.

Ikiwezekana mwambie akurekebishie maeneo yenye makosa kimuundo, ikiwa ni pamoja na kuandika upya aya au sura nzima *(usisahau utatakiwa kuongeza posho maana si rahisi watu hawa kukufanyia kazi bure hasa katika zama hizi za kila kazi ni biashara!)*
16. Tafuta mshauri wa kukuelekeza ni kampuni gani itaipokea aina hiyo ya hadithi; ila mara nyingi wataalamu wote wawili hapo juu wanawajua wachapishaji hao.
17. Tamati.

**Imeandaliwa na Shaaban Mngazija**

**Je; unataka kuhaririwa, kuandikiwa (ghost writing), kuhakikiwa au kuchapiwa hadithi au kitabu chako?**

**Wasiliana nasi kwa**
**Whatsapp: 0766974865**
**Call: 0672160016**

**Gharama zetu ni nafuu mno… mpaka mwenyewe utashangaa…!**

SALUM MAKAMBA

## USHAIRI NI BAHARI SI KIJITO - 03 -

**USHAIRI NI BAHARI SI KIJITO**

Sehemu ya Tatu

Baada ya kuonesha kwa ushahidi thabiti katika sehemu ya pili kuwa shairi linaweza kuwa na beti hata 100 na kuendelea sasa tutazame mambo mengine muhimu katika Ushairi ambayo baadhi ya watu hupotosha.

Kuna watu husema kuwa shairi ni sharti liwe na vina na mizani. Ati kwamba likikosa vitu hivyo linakuwa si shairi. Tena wapo ambao wameenda mbali hadi kuwakosoa watu wanaotumia "irabu" kama vina badala ya "silabi" wakiwaambia hakuna utunzi wa namna hiyo. Hawana rejeo lolote la maana katika madai yao hayo bali ni mambo waliyokaririshwa tu.

Ukurasa wa 53 katika Kitabu cha Kunga za Ushairi na Diwani Yetu (1979) Prof. M.M Mulokozi na Prof. K.K Kahigi wanasema, "Kanuni kuu ya utunzi wa mashairi ni uwiano kati ya fani na maudhui. Ndiyo roho na uti wa mgongo wa ushairi na fasihi nzima kwa ujumla. Ndiyo kigezo cha ndani cha ubora wa shairi."

Uwiano kati ya fani na maudhui ndiyo kanuni kuu, roho na uti wa mgongo wa ushairi. Siyo VINA NA MIZANI kama ambavyo baadhi ya watu hulazimisha.

Mshairi katika kutafuta uwiano wa fani na maudhui katika shairi lake anaweza akatumia vina vya silabi au asitumie ama asijihusishe kabisa na masuala ya vina na mizani na bado shairi lake likawa ni shairi bora kabisa

Katika ukurasa wa 54, Prof. Mulokozi na Prof. Kahigi wanasema, "Mtindo wa shairi ni tabia ya pekee ya utunzi au uandishi, na huhitilafiana kati ya mtunzi na mtunzi. Jambo hili hutegemea ufundi, hisia na unafsi wa mtunzi. Mtindo haufundishiki bali hutokana na uwezo na mazoea na vitabia pekee vya mtunzi."

Zingatia hapo kuwa "mtindo wa shairi huhitilafiana kati ya mtunzi na mtunzi na HAUFUNDISHIKI." Ina maana wewe kama unataka kutunga kama walivyokuwa wakitunga watu fulani hakuna shida lakini usianze kuwaambia watungao tofauti na hivyo wamepotoka au hawajui kumbe wewe ndiye una ufinyu na uchache wa elimu.

Katika kupigilia msumari kuwa utungo wa idadi yoyote ya beti unaweza kuwa USHAIRI na VINA na MIZANI ni mambo muhimu lakini si yenye maana sana Prof. Mulokozi na Prof. Kahigi wanasema katika ukurasa wa 54 na 55 kuwa, "Muundo ni mjengo wa shairi, yaani mfuatano wa vipande na beti, idadi ya beti, vituo, kujitosheleza, mtiririko wa vituko, wahusika, malumbano n.k.

Maudhui ndiyo yanayotuwezesha kupima umuhimu na manufaa ya shairi...yakiwa hafifu au yameparaganyika, VINA, MIZANI, tamathali na muundo (ikiwemo idadi ya beti) havitaufanya utungo fulani uwe shairi."

Kwa mantiki hiyo, mtu anaweza kutunga utungo kwa bahari moja, akaweka mishororo minne, vina na mizani na beti zisizozidi 12 lakini bado alichotunga kikawa si shairi kama MAUDHUI hayaoneshi umuhimu na manufaa ya shairi, ni hafifu au yameparaganyika (hayaeleweki).

Na kwa ufahamu huu, ndiyo maana wakati natoa maoni katika sharti alizozisema Hayati Prof. Nabhany niliandika, "Washairi wazingatie na kufuata kanuni hizo lakini zisiwabane. Wakiona kuna ujumbe muhimu wa kufikishwa kishairi lakini hauingii katika sheria hizo wasiutie mchagoni. Waandike na kuuleta nasi tutaupokea hivyohivyo."

Kwa nini niliandika hivyo?

Ni kwa sababu nilikuwa nafahamu kuwa maudhui yaliyobebwa na shairi yana umuhimu mkubwa kuliko mbwembwe nyingine kama idadi ya beti, vina na mizani, aina ya bahari, idadi ya mishororo na lugha itakayotumika.

*Inaendelea ukurasa wa 7*

# SAKO KWA BAKO:

## Christina Muhulo 'twilumba'– Fundi mitindo anayevijua vitabu

**Toleo letu la mwezi huu linatufikisha Kijitonyama. Hapa ninakutana na mwanadada ambaye nimetafuta siku nyingi sana ili tu kusikia neno kutoka kwake. Na safari hii, nimempata… hebu atuambie yeye ni nani?**

Mimi ni Christina Muhulo, au niite Twilumba Jamienda. Ni mzaliwa wa Iringa na ni mdau wa usomaji wa vitabu na kitaaluma ni mbunifu wa mavazi Jijini Dar-es-salam. Kazi yangu ninayofanya ni mbunifu wa mavazi na mshonaji wa nguo.

**Waoh! Swadakta, hapa sasa vitabu na mitindo ya nguo vimekutana. Hebu tuambie nini kilikusukuma kuwa msomaji wa vitabu?**

Malezi yalinifanya niwe msomaji wa vitabu. Nyumbani kwetu kulikuwa na shefu ya vitabu mbalimbali, palikuwa na vitabu hadi vya mapishi, Desturi ya hapo ndani ilikuwa Kila Jumamosi lazima shefu isafishwe na ni zamu ya watoto wote. Ni lazima utoe vitabu na upande. Sasa hapo ndio nikaanza kupata mshawasha wa kutaka kujua kilichomo ndani ya kitabu ndio ukawa mwanzo wangu wa kusoma vitabu nkiwa bado mdogo kabisaa.

**Doh! Sasa tuambie, kwa sasa usomaji wa vitabu unakusaidia nini na kazi yako?**

Vitabu sio kunisaidiaa tu bali vinanielimisha piaa kuhusu kazi yangu… **(kivipi?)** waandishi wa vitabu wanaumba wahusika na kuwavisha mavazi kutokana na mhusika anachofanya. Mfano anaandika: Frida alikuwa msichana mrembo mrefu na mweupe jioni ile alivalia gauni lake zuri la bluu lililomshika maungo yake, alipendeza sana.

Kama hivyo tunapata pointi mbalimbali

**Na huwa unapendelea viatabu vya aina gani?**

Vitabu vyote ninasoma, ila napenda sana Riwaya za kipelelezi haswaa.

**Kwanini?**

Navipenda kwa sababu vinaandika mengi tunayoyaishi kila siku pia vinachangamsha ubongo na Kuna ugunduzi mwingi kupita hivi vitabu.



**Kuna desturi ya wasomaji wengi wa vitabu kutaja idadi ya vile walivyosomaa kwa mwaka, hebu tuambie mwaka uliopita umesoma vitabu vingapi?**

Mwaka uliopita sijasoma vitabu vingi nimesoma vitabu 43 tu.

**Tupe mbinu ya ni vipi unafanikiwa kusoma vitabu namna hiyio?**

Nafanikiwa kusoma vitabu kwa sababu, nasoma vitabu vile vinavyovivutia, kuwa na Imani na baadhi ya waandishi unaowakubali kazi zao hazikupiti, kingine malengo napaswa kusoma ili nijifunze.

**Unawaambia nini wasiopenda kusoma vitabu?**

Kwanza nawapa pole! Napenda kuwaambia Kuna maisha ya kuishi ndani ya usomaji vitabu hivyo wanajinyima vitu muhimu sana katika maisha yao , wazinduke huko walikolala.

---

**Christina 'Twilumba' Muhulo, ni fundi mitindo mahiri hapa Tanzania. Ana weledi mkubwa sana wa ubunifu wa mavazi ya kila aina kwa wanawake na wanaume.**

**Je wataka kubuniwa au kushonewa nguo yako katika viwango vya juu? Wasiliana naye kwa -**

**Whatsapp au SMS 0786679805**

# MSALITI - 05

Na. Richard Mwambe



***Ilipoishia...***

**"Najua, na nitamjibu hivihivi… hata kama atakasirika na kuamua kunivua wadhifa wangu, nitamjibu hivihivi…" akameza funda la mate na kuendelea, "Sana sana nitamshauri tuombe vyombo vya uchunguzi kutoka nje ya nchi," akahitimisha jibu lake.**

***Endelea...***

Mazungumzo ya wawili hawa yalichukua kama nusu saa hivi. Walipotahamaki giza lilishaanza kutafuna nchi, wakaagana na kila mmoja akaondoka zake. Hapo walipoketi palikuwa ni chumba maalumu ndani ya *Officers Mess*. Habari za vifo vya wanajeshi wale zilitawala vyombo vya habari ndani na nje ya nchi kwa takribani majuma mawili, tangu tukio lilipotokea na hadi miili ile ilipofikishwa nchini. Ilitia uchungu kweli kweli, lakini hali ilikuwa kama ilivyo. Ni mwandishi mmoja, kati ya waandishi wote waliokuwa wakiripoti habari ile aliyependwa na wafuatiliaji, maana alikuwa akijua kuichambua kwa kina na kufikia kuwahoji watu wazito juu ya kazia hiyo.

Lakini kitu pekee kilichowashangaza watu ni kwamba, habari iliyotoka siku iliyofuata juu ya kuwasili na maazishi ya kijeshi ya marehemu wale, haikuwa na utamu wa uandishi wake. Kila msomaji aliona *'hapana'* mwandiko huu siyo wake. Vifo hivyo viliteka hisia za kila Mtanzania.

❦

Siku iliyofuata, Kamanda Amata aliingia ofisini kwake kama kawaida. Gina alikuwa keshatangulia saa moja kabla. Na ndivyo ilikuwa desturi yao. Alipoingia na kutundika koti lake kwenye kiangio akageuka na kumsalimia huyo mrembo.

"Naona himahima leo vipi?" Gina akamuuliza Amata.

"Aah! Mambo hayaishi duniani hapa aisee…" Amata akajibu huku akivuta hatua ndogo ndogo kuelekea mlango wa pili ambao kwawo ndipo ungeingia katika ofisi yake. *AGI Investment* ilikuwa kampuni ya kufanya *clearing and forwarding*, lakini siri ya kampuni waliijua wafanya kazi hawa wawili. Mizigo waliyokuwa wakiishughulikia waliijua wao tu na wenzao wachache.

"Jana si umepumzika vya kutosha?" Gina akauliza.

"Nipumzike wapi? Yaani hekaheka haziishi, kuna jambo jipya limezaliwa, hebu njoo huku tuyajenge, usiache kikombe cha kahawa tafadhali," Amata akamwambia huku yeye akiingia ofisini kwake. Dakika kama tano baadaye, Gina aliungana na bosi wake na kuketi kwenye kiti kingine kilichowafanya watazamane. Kikombe cha kahawa na chai vilikuwa kati kati yao na biskuti kadhaa.

"Niambie…" Gina alianza.

"Jana nimepokea simu yenye utata kidogo pindi tu nilipoingia nyumbani… utadhani mpigaji alikuwa ananisubiri nifike," akasema huku kikombe kile cha kahawa kikiwa jirani na kinywa chake. Harufu ya kahawa hii safi kutoka Mbinga ilizifariji pua zake.

"Inahusu nini?"

"Sasa hapo ndo utata wenyewe ulipo. Mpigaji alionekana kama yupo kwenye hali mbaya ama ya mateso au sijui nielezeje, alinambia tu anataka kunipa habari lakini hakufanikiwa na ile simu ikakatika," Amata akaeleza.

"Mh! Kumekucha…" Gina akasema.

"Tena na makucha yake!"

"Jina lake alifanikiwa kutaja? Maana walau inabidi tuwe tunawahi kuuliza majina," Gina akataka kujua, na kuongeza maneno kidogo. Akainua chai yake na kupiga funda moja kisha akatua kile kikombe chini kwa madaha.

"Alijitambulisha kwa jina moja tu Besta, halafu ndipo simu ikakatika. Usiku uleule nilipofanya uchunguzi wangu nikapata majibu kuwa ile simu imepigwa kutoka Ngara na ni mali ya Innocent Jonathan Kabelwa… umewahi kulisikia hilo jina?" Amata akasema kwa katupa swali kwa Gina.

Palikuwa na ukimya wa namna fulani. Ukimya ambao ulidhihirisha kukosekana majibu ya haraka juu ya kadhia inayozungumziwa au kurudisha kumbukumbu ya aina fulani. Kimsingi kama wanausalama walitakiwa kunusa kila harufu yenye mashaka, si ile nzuri pekee toka kwenye Kahawa ya Mbinga iliyokuwa mezani pao. Sekunde kama 30 hivi ukimya ule ukaonesha dalili ya kupigwa teke. Gina alikuwa kama mtu anayekumbuka jambo hivi. Akainuka na kuondoka mle ofisini kwenda chumba kingine bila kuaga, kisha dakika moja baadaye akarejea na gazeti mkononi.

"Humu kuna Besta sasa sijui kama kuna mahusiano na huyo aliyekupigia simu," Gina akaeleza na kuweka gazeti lile mezani pale. Gazeti hilo lilikuwa MZIZIMA LEO, toleo la wiki jana tu. Katika

# MSALITI - 05



ukurasa wake wa mbele lilibebwa na kichwa kizito cha habari, 'WINGU ZITO LATANDA TANZANIA' halafu kukafuatia na dondoo chache ndogo ndogo *'Kwanini Wafe Watanzania tu?'* likikuwa swali la kwanza, kisha likafuatia swali jingine, *'Nani Amfunge Paka Kengele?'* . Swali hilo la pili lilinukuu kauli ya zamani ya Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere.

"Kwanini wafe Watanzania tu?" Amata akamuuliza Gina.

"Inawezekana Besta ndiye mwenye jibu… mwandishi anaitwa Besta Ekolaneza" Gina akajibu. Amata akabaki kimya kwa jozi la sekunde.

*Besta Ekolaneza!* Akawaza.

"Inaweza kuwa ni yeye?" akauliza Amata.

"Sijajua nimejaribu tu kuunganisha *dots*," Gina akaeleza huku akiweka lile gazeti kando na kuendelea kuongea, "Unaonaje tukimtembelea Mkurugenzi wa Mzizima Leo? Hili si ni gazeti binafsi tu… waonaje?" Gina alipendekeza wakati tayari Amata alikwishanyanyuka. Safari ya wawili hao ikaanza. Wakati mwingine walipenda kujijibu maswali kwa vitendo badala ya maneno. Kwani sekunde moja kwao ilikuwa na thamani kubwa sana.

❦

Katika ofisi za gazeti la MZIZIMA LEO, ndani ya chumba kimojawapo alikuwamo Mkurugenzi wa chombo hicho Hamidu Bakari Mpelembwa. Aliketi ofisini humo akisoma baadhi ya habari zilizomfikia huku sikio lake likiwa kwenye kikao cha Bunge kilichokuwa kikirushwa kupitia runinga iliyowekwa juu ya kabati mojawapo. Alipopewa taarifa ya ugeni huo akaruhusu uingie. Amata na Gina wakakaribishwa vitini na kuketi.

"Karibuni sana, naweza kuwasaidia?" yule mkurugenzi akauliza huku akionekana kupumua kwa shida kutokana na mwili uliomshinda nguvu. Baada ya maamkiano na utambulishano wakaendelea. Gina akatoa lile gazeti na kuliweka mezani, yule mkurugenzi akalivutia kwake na macho yake yakatua juu ya kichwa cha habari ileile.

"Tuna shida na huyu mwandishi machachari," Amata akaeleza.

"Na ni machachari kweli… mnataka kuniibia mwandishi wangu?" yule mkurugenzi akauliza kwa utani.

"Sivyo, kuna kazi kidogo tunataka kumwomba atusaidie, tunajua kuwa yeye anaweza kutupatia taarifa sahihi kutokana na kazi yake," Amata akaeleza.

"Taarifa gani, naweza kujua?" akauliza yule mkurugenzi.

"Kama tulivyokwambia kuhusu kampuni yetu, sisi tumepokea mzigo hapa kontena mbili ambao unatakiwa kuchukuliwa na mwenyewe ambaye ni singa singa raia wa Zambia. Tatizo linalokuja tangu tuupokee hapa katika bandari yetu, miezi mitatu sasa tunazungushwa tu kuutoa ule mzigo. Mwenye mali kafika mpaka hapa lakini hakufanikiwa kukamilisha hilo suala… sasa kuna nini bandarini? Huyu Besta Ekolaneza anaweza kufanya utundu wake akaumbua watu pale…" Amata akatunga stori palepale ili tu kuteka mawazo ya bosi huyo.

"Mmmh! Sasa ninyi mnataka kumtafuta nyoka miguu… mnajua kuwa masuala ya bandari ni masuala nyeti sana! Yaani ukiyagusa, umeigusa serikali na wenye madaraka. Inawezekana kwenye hayo makontena kuna mizigo isiyo halali kwani hawakukuambieni kuna nini?" akahoji mkurugenzi yule.

"Ile mizigo ni vyombo vya nyumbani tu…" Gina akadakiza.

"Heeeh! Vyombo tu aaaaahh au na nyie mna mkono mfupi?" yule mkurugenzi akauliza baada ya kushangaa huku akijiweka vizuri pale kitini. ***Itaendelea...***




Kitabu MSALITI kipo madukani, jikamatie nakala yako kwa Tsh 15,000 tu.

Tembelea duka la Kona ya Riwaya Kinondoni au piga

**simu namba 0655428085**
**Whatsapp 0766974865**

Jikamatie nakala yako sasa

# HADITHI: Najutia Kuwa na Wewe—05



**MTUNZI: ASHA SIRAJ**
**Whatsapp 0789044345**

**UTANGULIZI**

**Mapenzi sio kitu cha kuwekea maanani sana kwasababu ipo siku yanaweza kukuletea shida huko mbeleni, kuna baadhi ya changamoto nyingi hutokea. Hivyo ukisema kila jambo uliwekee maanani basi mapenzi yako yatabaki kuwa na majuto siku zote. Kutana na binti SHAZMA aliyepitia mateso mengi kwenye mapenzi yake na kujikuta akijutia kwanini amkabizi moyo wake mwanaume asiye na fadhila**

***Ilipoishia…***

**Sauti iliyosika pembezoni mwangu ikiniomba kunivusha niligeuka haraka nakutaka kujua ninani huyo anayeniomba kinivusha barabara, Mungu wangu alikuwa kijana yule tuliyemuacha dukani kwanza nilibaki nimeduala huku roho yangu ilienda mbio.**

***Songa nayo...***

Niliogopa sana pale alipounyoosha mkono wake akiniomba nimshike kwa ajili ya kunivusha. Nilianza kubisha ila mwisho nilikubali mwenyewe haswa pale nilipoona magari yakipita kwa kasi.

Niliona nikiwa mbishi basi mwisho wangu unaweza kuwa hapa. Weee, nani anataka kufa kifo cha kujitakia? Niliushika mkono wake, huku upande wa pili Judithi akiwa anachekelea tu!

Kama nilimwambia nina shida na ile mimeno yake kama mihogo iliyoanikwa juani. Taratibu m-kaka huyo alinisogeza karibu yake huku tukiwa tunapiga hatua kuelekea upande wa pili. Ila nijihisi tofauti pale niliposhikwa mkono na kijana huyo. Roho yangu ilinienda mbio mpaka nikawa najiuliza hivi ninashida gani mimi?

Kipindi hicho ulikuwa mwezi wakumi na mbili tunaelekea wa kwanza, nilikuwa *form three* tulikuwa tumebakisha miezi kadha kuhitimu pale *secondary*.

Basi bwana baada ya kufika upande wa pili aliniachia mkono wangu nikabaki kumshukuru tu.

“Jamani asante sana kaka kwa msaada wako, “

“Usijali binti, mimi naitwa Shahdu” alijitambulisha mwanakaka huyo. Nikabaki kukodoa macho, “nashukuru sana Shahdu kwa msada wako, mie naitwa Shazma,” nikasema.

“Oohhh mashallah jina zuri sana,” akasema.

“*Wow Shazma and Shahdu* hadi raha majina yenu yanaendana sana,” aliongea Judithi nikatamani kumpiga kibao.

“Ni sawa sio mbaya,” alijibu Shahdu huku akitabasamu.

“Haya Shahdu sisi tunaomba kuondoka hata hivyo tumeaga shule kwa *matron* naogopa anaweza kutuadhibu maana mda umekuwa mwingi sana”.

“Ohh kumbe bado mnasoma?”

“Ndio usione huu mwili wangu niliokuwa nao ukadhani mimi nim mkubwa hapana, huu ni mwili tu ila bado tunasoma,” nikamwambia.

“Ok sawa niwatakie masomo mema,” aliongea Shahdu mimi nikashindwa hata cha kumjibu.

Judithi alidakia, “tunashukuru sana kukutana na wewe naomba hata siku nyingi tukutane tena”.

“Msijali milima haikutani ila binadamu hukutana”, aliongea Shahdu huku akiwa anatabasamu. Tabasamu lake lilinikosha sana.

Niliamua kumvuta mkonoJudithi ili tuweze kuondoka nilihofia mambo yanaweza kuwa mengi hilo nitabasamu tu nikiendelea kukaa pale basi nitajikuta navutiwa na vitu vingi kwake

Tuliondoka akabaki kucheka tu, nahisi alihisi leo nimekumbana na machizi hapa. Basi tuliondoka sikutaka tena kusikia habari za kudhurura. Judithi alifosi tukazurule ila mimi sikuwa tayari kwa sababu ya kumhofia *matron* huku shule. JJudithi aliongea “huu ni mda wa sisi kuzurula hatutopata tena mda mwingine tukishaingia ndani ya geti lile”.

“Aaahh vyovyote bwana naomba tuondoke”.

Ni kama Judithi alinuna ila mimi sikujali kabisa, niliongea “nuna kikikuisha utarudi kwenye hali yako,” nahisi alitamani hata kuning’ata ila hakuwa na uwezo ilimbidi atulie kama moja.

Baada ya dakika kadhaa tuliwasili pale shule, tulimkuta *matron* akiwa

amekaa kwenye kiti. "Ilikuwa kidogo mkute adhabu yenu hapa," aliongea *matron*. Mimi nikageuza macho yangu na kumtazama Judithi aliyeg'ang'ania tukazurule.
"Samahani sana *matron* dukani kulikuwa kuna watu wengi hivyo ilibidi tuvute subra kidogo" nikaomba radhi. "Ni sawa ila nashukuru amjanivunjia heshima maana nilikuwa nawaza msije kwende kutafuta vijana huko",
"Jamani *matron* sisi hatuko hivyo", niliongea hivyo, nikamkumbuka *handsome* wangu aliyenivusha barabara mda mchache uliopita.

Tuliondoka kuelekea bwenini, tulikaa zetu na kuanza kupiga stori mbili tatu, "unajua nini Judithi, yule mkaka nikama nimemuelewa hivi!"
Niliongea hivyo judithi akabaki kunicheka tu! "Cha ajabu kipi kinachokuchekesha? ambacho huelewi nini kumuelewa au?"
"Ya kwangu macho shoga mmhh kwa jinsi vile alivyokushika akikuvusha barabara ndo ukachaganyikiwa hivyo?"
"Vyovyote vile, mi sitaki kujua ila mimi nimemuelewa gafla yaani," nikaeleza.
Sikuwa na rafiki mwingine pale shule zaidi ya judithi tu, alikuwa mtu wa karibu yangu sana, sikuweza kumficha kitu kuhusu mimi, hata yeye pia hakuweza kunificha chochote kile kinachomuhusu.

Kiufupi tulikuwa kama ndugu hivi, tulifanya kile ambacho tulikiona sahihi kwetu, tulisaidiana kwa kila jambo japo hatukuwa na maisha ya kivile ila upendo wetu ulikuwa tosha kwenye maisha yetu.
Siku zilizidi kusonga mbele ila sura ya yule kijana haikuisha kwenye macho yangu, sijui kama na yeye alikuwa ananifikiria au laah!

****


Ni miezi mitatu imepita sasa sijawahi kukutana naye tena na nilisahau kumuuliza ni wapi anaishi, sijui kama alikuwa ameoa au lah. Nilibaki kumfikiria yeye tu na hivo nilikuwa sijawahi kumpenda mtu ndo kabisa.

Nilizidi kuchanganyikiwa kwasababu yake, hadi niliogopa kwani ilikuwa ghafla iweje nimemuona mtu huyo kwa mara ya kwanza ndo tayari nishampenda.
Ikiwa hata tabia hizo sikuwa nazo, ila hisia huwa ni mwanaharamu yeyote atayetokea mbele yako basi utahisi umemuelewa.
Nilijitahidi kumpotezea ila sura ya kaka huyo ilikuwa inanijia mara kwa mara kwenye taswira yangu, nilijiweka *busy* kwenye masomo yangu kusudi niweze kumsahau mkaka huyo.
Nakumbuka tulikuwa tumebakisha miezi kadha kufanya mtihani wa mwisho pale shule hivyo nilikuwa silali usiku kwa ajili ya kujisomea.
Nakumbuka yalikuwa majira ya saa sita nikiwa *busy* nakujisomea wakati huo Judithi alikuwa amelala huku akikoroma kama nyoka vile.

Nilimsohelea nakwenda kumtingisha niliona kabisa ananikera kwa yale makelele yake ya kukoroma, "Judithi uwe unalala vizuri unajua kabisa ukilala chali madhara yake, yani unakoroma hadi nashindwa kusoma vizuri." Judithi alinijibu, "huko kusoma ndo unadhani utakuwa wa kwanza darasani, hata huyo rais hakuwa anasoma hivyo yani nyie mnaojifanya kusoma-soma ndo unakuta kwenye mtihani Amna kitu Em' niache mimi nikorome zangu mimi," akanijibu. Nilitamani kumzaba kibao maana hata alichokiongea hakuwa anajielewa vyovyote vile.
Nilijiondokea pale na kumuacha na ubishi wake. Siku hiyo nilisoma sana hadi nikajikuta nachoka mgongo, baada ya kuona nimechoka sana niliamua kuacha na kwenda kulala. "Nakuona rais mtarajiwa!" huyo aliongea Catherine aliyekuwa amelala karibu na kitanda changu.

Sikumjibu kwa sababu namjua vizuri yeye huwa ni mtu wa ugomvi, sio kwamba nilikuwa namuogopa bali sikutaka kuamsha ugomvi alafu ukiangalia ulikuwa usiku wa manane.
Nilisogea hadi sehemu nilipokuwa nalala nilipanda ngazi kuelekea kitanda cha juu kabisa maana yeye alikuwa analala mwanzo kabisa huku katikati alikuwa analala Judithi mwisho nilimalizia mimi.
Nilivuta shuka langu nakujufunika huku nikajirabu kuutafuta usingi mnono, ila cha kushangaza siku hiyo ilikuwa siku....

***Itaendelea….***



Kisha Alibaba alienda jikoni na kumkuta Marjane.

"Tuna mgeni kwaajili ya chakula cha jioni leo," alimwambia. "Jina lake ni Khoja Hussein, ni mfanyabiashara mkubwa sana wa vitambaa vya hariri. Ni rafiki wa Khalid pia. Hawezi kula chumvi, hivyo usiweke chumvi katika chakula. Tafadhali pia pika mbogamboga – na kumbuka kutokuweka chumvi kwenye mbogamboga pia."

"Sawa bosi," alijibu Marjane. Kisha akanyamaza kidogo. "Huyu Khojha Hussein ni nani?" alijisemea moyoni. "Kwanini hali chumvi?" kisha Marjane akakumbuka usemi wa kizamani unaosema kwamba: ***ukitaka kumwua mtu, usile chumvi nyumbani kwake.*** Ghafla Marjane akaingiwa na hofu. "Khoja Hussein amepanga kufanya nini?" alijiuliza. "Bosi wangu Alibaba yuko hatarini?"

Alipomaliza kuandaa chakula, alibeba sahani ya kuku mpaka mezani. Alipokuwa akiiweka mezani, Marjane alimuangalia Khoja Hussein kwa makini sana wakati akiwa anazungumza na Alibaba na mkewe.

"Huyu mtu mwenye ndevu ndefu nyeusi na upara," Marjane alijisemea moyoni. "Lakini namtambua huyu mtu – ni kiongozi wa wezi – muuza mafuta – na sasa ni muuza vitambaa vya hariri!! Bosi wangu yuko hatarini tena – huyu mtu ana mpango wa kumuua bosi wangu usiku wa leo! Lazima nifikirie mpango madhubuti."

Marjane akarudi jikoni na kuleta sahani ya mikate na bakuli kubwa la wali na mbogamboga. Alipokuwa akivitenga mezani, akamuangalia mgeni tena wakati akizungumza na Khalid na mke wa Kassim.

Ghafla Marjane akaona upanga. Ulikuwa umefichwa kwenye koti la mgeni! "amejaribu kuficha upanga," Marjane alijisemea moyoni. "Lakini nimeweza kuuona."

Alipokuwa anamalizia kutenga vyakula vilivyobaki, alizidi kufikiria zaidi kuhusu mpango wake.

Walipomaliza kula kuku, Alibaba akasema, "Kuleni matunda. Haya maembe ni mazuri sana."

"Ahsante," alijibu Khoja Hussein. Kisha akachukua embe moja kutoka kwenye bakuli na kuegemea kwenye kiti chake na kunyoosha miguu yake mbele na kutabasamu.

"Chakula cha leo ni kitamu sana," alimwambia Marjane. "Wewe ni mpishi mzuri sana. Niambie, mbali na kupika nini kingine kizuri unaweza kufanya?"

Sasa Marjane akapata nafasi ya kutimiza mpango wake.

"Ninaweza kucheza," Marjane alijibu. "Ungependa nicheze uone burudani wakati unakula matunda?"

"Unasema..??" alisema Khoja Hussein, akamgeukia Alibaba. "Je Marjane anaweza kucheza tumuone?"

Alibaba akatabasamu na kuitikia kwa ishara ya kichwa . Alikuwa na furaha kuona mgeni wake anaburudika jioni ile.

"Uhakika kabisa," alisema Alibaba. "Na atatupigia dufu pia. Anajua sana kupiga dufu. Nenda kajiandae Marjane."
"Sawa bosi," Marjane alijibu.

Marjane akaenda chumbani kwake. Akavaa gauni refu la rangi ya fedha lenye kung'aa kwa juu. Akajifunga kitambaa mdomoni kuzunga kichwa chake. Akavaa mkanda mnene kiunoni. Kutoka kwenye mkanda ule akaweka ala ya kuwekea kisu, na katika ala ile akaweka kisu. Kisha akachukua dufu na kutoka chumbani kuelekea sebuleni kwaajili ya kucheza.

"Huyoooo amependeza!!" Alibaba alisema kwa furaha. "Sasa tutaburudika!"

Marjane akasimama katikati ya mlango na kuinama kidogo kama ishara ya kusalimia.

"Ingia! Cheza, Marjane!" Alibaba alisema kwa furaha. "ingia na ucheze! Mgeni wetu aone jinsi unavyojua kucheza!"

Marjane akaanza kupiga dufu taratibu na kuanza kucheza akizunguka chumba kile huku akitabasamu.

***Itaendelea...***



# DIRISHA LA TUZO YA KITAIFA YA MWALIMU NYERERE YA UANDISHI BUNIFU MSIMU WA NNE LAFUNGULIWA

*Na mwandishi wetu.*

Kupitia kikao cha ndani kati ya Waziri wa Elimu, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) na waandishi bunifu pamoja na wadau wa fasihi nchini kilichofanyika tarehe 6 Agosti mwaka huu katika ukumbi wa Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam (UDSM), mwenyekiti wa Kamati ya Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu, Profesa Penina Mlama ametangaza kufunguliwa kwa dirisha la Msimu wa nne wa Tuzo hiyo.

Akizungumza katika hotuba fupi ya ufunguzi huo, Profesa Penina Mlama alitanabahisha kuwa, katika msimu wa nne wa Tuzo hiyo tanzu zitakazoshindaniwa ni Riwaya, Ushairi, Tamthiliya na Hadithi za Watoto.

Aidha alisema kuwa, vigezo vya ushindani katika Tuzo hiyo msimu huu wa nne vitatangazwa rasmi kupitia kurasa za mitandao za Taasisi ya Elimu Tanzania na Tuzo Nyerere siku za usoni na miswada hiyo itaanza kupokelewa rasmi tarehe 15 ya Mwezi wa Agosti na makataa yake yatakuwa tarehe 30 Novemba 2025.

Naye Waziri wa Elimu, Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda (Mb) alisema katika hotuba iliyotangulia kuwa lengo la tuzo hiyo ni kukuza uandishi bunifu, kukuza Kiswahili na kukuza soko la vitabu hapa nchini.

Kikao hicho kilichowakutanisha wadau hao wa uandishi bunifu kilikuwa na lengo la kutathmini tulikotoka na nini kifanyike ili kuboresha tuzo hiyo ya kitaifa.

Tuzo hii iliyoanzishwa miaka minne iliyopita imeleta chachu ya kiushindani katika uandishi bunifu ambao hapo awali ulionekana kusinzia. Fauka na hayo, inaleta ari mpya ya usomaji wa vitabu mashuleni kutokana na upatikanaji wa vitabu vipya vitakavyopitia kwenye Tuzo hii.

Ngurumo ya mwandishi inawatakia kila la kheri waandishi bunifu kote nchini katika kinyang'anyiro hicho, kilichotajwa kuwa kilele chake ni tarehe 13 Aprili ya 2025.



Profesa Adolf Mkenda (MB), Waziriwa Elimu Sayansi na Teknolojia.



Profesa Penina Mlama, Mwenyekiti wa kamati ya Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu.

# HISTORIA YA VITABU ULIMWENGUNI—5

*Na Mwandishi wetu*

Bado tunaendelea na uchambuzi wetu wa historia ya vitabu, ambamo tumeona na kupitia vitabu vya kale ambavyo mwanadamu alivitumia katika vipindi mbalimbali vya maisha yake.

Leo basi, tutakitazama kwa kifupi Kitabu cha Wafu cha Kimisri yaani The Egyptian Book of the Dead.

Hiki si kitabu kimoja tu kama tunavyofahamu vitabu vya leo, bali ni **mkusanyiko wa maandishi ya kidini na ya kifalsafa** yaliyokuwa yakitumika katika **mazishi ya Wamisri wa kale**, hasa kwa watu wa heshima au wenye uwezo kifedha. Kimsingi, ni mwongozo wa kiroho kwa marehemu kuelekea maisha ya baada ya kifo.

## Maelezo Muhimu Kuhusu *The Egyptian Book of the Dead*:

- **Jina la Kiasili:** Wamisri hawakuliita kwa jina hilo. Waliliita kwa jina linaloweza kutafsiriwa kama *"Maneno ya Kuondoka kwa Mwangaza"* (*"The Book of Coming Forth by Day"*).

- **Lengo:** Lilikuwa ni kusaidia roho ya marehemu **kupita salama ulimwengu wa chini (underworld)** hadi ifikie maisha ya milele. Lilieleza mambo kama:

- Namna ya kuzungumza mbele ya miungu
- Majaribio anayopitia marehemu
- Hukumu ya moyo (Anubis akipima moyo dhidi ya uzito wa "ubora wa haki")
- Kuingia kwenye uzima wa milele

**Yalikuwa yakiandikwa wapi?** Kwa kawaida maandishi haya yaliandikwa kwenye:

- **Ukuta wa kaburi**
- **Papyrus** (karatasi za kale)
- **Vifaa vya mazishi** kama vile masanduku ya maiti

**Lugha iliyotumika:** *Hieroglyphics*, lugha ya picha ya Wamisri wa kale.

**Yaliyomo:** Yana maombi, nyimbo, ramani za kiroho, na maagizo ya namna ya kujilinda dhidi ya roho wabaya na mitego ya ulimwengu wa chini.

## Je, Kuna Mafundisho ya Kiroho Ndani Yake?

Ndiyo. Ingawa si ya dini za leo kama Ukristo au Uislamu, maandiko haya yana:

- Maadili ya maisha mema
- Imani ya haki, uwazi, ukweli, na kutotenda mabaya
- Maandalizi ya maisha baada ya kifo — jambo ambalo linafanana na mafundisho ya kiroho katika dini nyingi za leo.

Katika toleo lijalo, tutaangalia kwa kifupi kitabu

TANGAZO



Niliyopata Kutoka Kitabuni
**Kitabu** : Mtu Mwenye Furaha Zaidi Duniani
**Mwandishi:** Eddie Jaku

Eddie Jaku alikuwa Myahudi mzaliwa wa Ujerumani aliyenusurika mateso ya Holocaust, haya ni mauaji ya halaiki ya Wayahudi zaidi ya milioni sita na wengine wengi waliouawa na utawala wa Nazi wakati wa Vita Kuu ya Pili ya Dunia. Licha ya mateso, Eddie aliishi maisha marefu kwa furaha na akaandika kitabu The Happiest Man on Earth, ambacho kinaifundisha dunia kuhusu matumaini, wema, na nguvu ya kushukuru. Hapa kuna mambo machache muhimu kutoka kwenye kitabu hiki:

**1. Furaha Ni Uamuzi**
Kichwa cha kitabu si utani bali ni falsafa ya maisha ya Eddie. Alipitia mateso makubwa, lakini bado aliamua kuwa mwenye furaha. Anatufundisha: maumivu hayaepukiki, lakini huzuni ni hiari. Yaani, hata wewe unaweza kukumbwa na hali ambayo usingeweza kuizuia isikutokee, lakini bado unaweza kuamua kuwa na furaha unapoitafutia suluhisho.

**2.Chuki Ni Gereza Halisi**
Eddie alisema, "Sikuwahi kutaka Hitler ashinde." Licha ya kupoteza familia, uhuru, na kuishi katika mateso, Eddie alikataa kuwa chombo cha chuki au huzuni ya milele. Hitler alilenga kuwaangamiza Wayahudi pamoja na kuua furaha na matumaini yao. Hata hivyo, Jaku anasema kuwa Hitler hakufanikiwa kuvunja moyo wake, kumuondolea utu wake, wala kumnyima uwezo wa kupenda na kuwa na matumaini tena.Chuki humfungia mwathirika, si mtesi. Sisi kama binaadamu kuna mambo yanayoudhi sana na tunachukia, ni vema kuwa na hisia na kuzionesha ila ni vema zaidi kuweza kuzicontrol ili zisikuharibie ratiba.. mtu akikukwaza tafuta namna ya kwenda mbele bila kupoteza mda.

**3.Wema Ni Uasi wa Kweli**
Katika Auschwitz, moja ya kambi za mateso na mauji, kugawana kipande cha mkate ilikuwa ni kuhatarisha maisha, lakini bado Eddie aliona watu wakifanya hivyo. Funzo gani alipata? Binadamu anaishi kupitia matendo madogo ya upendo, hasa yale yasiyo na mantiki. Kwa hiyo usiache kufanya matendo madogo madogo kwani hayo huacha alama kubwa. Nina ushaihidi mimi binafsi Anna.

**4.Shukrani Ni Mstari wa Uzima**
Eddie aliendelea kuishi kwa kushukuru mambo madogo: machweo ya jua, kurudisha tabasamu lililopotea. Kauli yake: "Amka kila asubuhi na tafuta jambo moja zuri la kuthamini." Furaha hukua pale shukrani inapopandwa. Hata leo, kwanza shukuru kwa kuweza kusoma ujumbe huu alafu ona jinsi ambavyo moyo wako utaongeza mapigo mazuri.

**5.Uzuri wa Maisha Unaongezeka Unapokaribia Kifo**
Hili lilimfundisha Eddie kuthamini mambo ya kawaida kama vile kula chakula cha moto, kufurahi na marafiki, na kadhalika. Alitoa funzo kuwa ni vyema kuchukulia kila siku kama zawadi ambayo unakaribia kuipoteza. Naomba na wewe kila siku ya maisha yako ifanye iwe ya furaha, usisubiri hadi uugue ndiyo uanze kujilaumu oooh ningejua nilipokuwa mzima ningefanya hili au lile.

Kitabu hiki si tu simulizi, bali kinakuwezesha kutafakari kuhusu maisha.


Kusoma vitabu kwa urefu wake, jiunge na maktaba yetu:-

Anna Mbise Pan-African Mobile Library Tanzania@everyone ili uwe mwanachama na upewe vitabu bure.

Karibu!

Anna Mbise (Chuganese)
7 Julai 2025, Dar

**0746359536**



# HABARI PICHA




Picha ya pamoja katika uzinduzi wa kitabu cha Living With Cancer cha Prof. Mwandosya



'Mkwe wa Jaji Mkuu' mikononi mwa Wafula wa Wafula, kutoka Kenya (picha kutoka mtandaoni)



**Pichani chini: Prof. Joseph Mbele (katikati) kwenye picha ya pamoja na mama na binti**



Picture caption



**TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.**
**Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.**
**Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

## NDIYO KURASA YA MWISHO

Hatima kutamatika, kwa kitabu cha maisha
Uzima ukikatika, kila tabu zinaisha
Kupima kwa uhakika, kitabu kukichapisha
Ndiyo kurasa ya mwisho.

Kitabu chenye kurasa, za hekima na upendo
Si tabu kukitakasa, kwa heshima za matendo
Adabu inatuasa, tukizima kwenye mwendo
Ndiyo kurasa ya mwisho.

Kurasa ya ukumbusho, wazikaji watazikwa
Anasa ni miyeyusho, mahitaji kufunikwa
Yapasa tufushe fusho, watendaji tukishikwa
Ndiyo kurasa ya mwisho.

Haijalishi ni nani, kurasa ya kusubiri
Haitishi kwa imani, inatisha kiakili
Tarishi kama shetani, usipagawe na mwili
Ndiyo kurasa ya mwisho.

Kurasa yake Ndugai, imefungwa kwao Kongwa
Kurasa ya bai bai, imetungwa bila nongwa
Thamani yetu uhai, wagongaji watagongwa
Ndiyo kurasa ya mwisho.

Andika kitabu chako, kuchuma vyema vizuri
Ikifika zamu yako, hakuna tena kiburi
Utazikwa peke yako, kuhema kwenye kaburi
Ndiyo kurasa ya mwisho.

**Na: Mfalme wa Tungo Tata**
**T King Control**
**Dar es salaam**

## NIMEMISS PISHILE

Nakumbuka pishile
Lenye utundu bwelele
Alinipa peke nile
Nile kisha nile

Kwa ufundi alipikale
Manjonjo yalinogile
Mandalizi ya pishile
Kwangu nibaki hoile

Kitumbua safi mchele
Pajaze dimwe dimwele
Uno feni fenile
Mipya mizungupule

Kele-kele kelele
Jirani alaanile
Mimi nafaidile
Yeye anunele

Nilipotwanga kinule
Na kusaga haragele
Nikasikia kelele
Mwali kapiga ndwele

Utamu hadimule
Wapi nitapatale
Nimemiss pishile
Pishi la Kimanyemale.

**Amata Ric**
**(Mate ya Simba)**
**Iringa**


**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**

# TANGAZO













Jenga tabia ya kusoma vitabu kila upatapo muda. Vitabu vyetu vinapatikana

Duka la Kona ya Riwaya Kinondoni - Simu namba 0655428085
Posta Mpya Dar es salaam karibu kabisa na mzunguko wa Sanamu ya Askari kwa Joji - Simu 0713454152
Morogoro Morena hotel, Stendi ya Dalala Smaki Samaki na Bima kwa Markus Mpangala - Simu 0719226293
Au wasiliana nasi Jamvi la Simulizi kwa Whatsapp Namba 0766974865

# KUTOKA MAKTABA:MAISHA NI MAPAMBANO—11

**Hiki ni kitabu kilichoandikwa miaka mingi sana nyuma. Kiliandikwa ili kiweze kusomwa na watu mbalimbali na kuwekwa kwenye maktaba za vijijini. Tunakitoa kutoka kwenye maktaba yetu ili kukupa uhondo, Ngurumo ya Mwandishi ni kisima cha fasihi chenye hazina iliyotukuka.**

"Asiyefunzwa na wazazi, hufunzwa na ulimwengu". Au Asiyesikia la ,kubwa huvunjika…….". Hayo yote ni mabaya ambayo hujitatua yenyewe. Lakini siyo ujinga! "Dawa ya ujinga ni kisomo tu". Alikuwa akikariri Mpepo na kuongeza kusema kwamba ipo siku ujinga utajimaliza wenyewe na iwe mazungumzo baada ya habari au ndoto.

Mama Tabu alijiunga na kisomo pamoja na wanakijiji wengine wengi. Kwa vile Mpepo alikwishapiga hatua alikuwa akimsaidia mkewe kumsomesha saa za jioni na kumshirikisha kusikioliza redio. Vilevile alikuwa akimsomea hadithi za vitabu mbalimbali, hadithi ambazo zilimtia mama Tabu hamu na shauku ya kuchukua muda mrefu kujifunza.

Baada ya kumaliza kisomo alijiunga na darasa la maarifa ya nyumbani. Mapishi aliyapenda mno. Kila walipokuwa wakizungumza mara nyingi mara nyingi hawakuacha mapishi. Ilifika hatua ambapo wakizungumzia mapishi mtu mwingine yafaa asogee mbali maana mate na njaa vitaanza kumtoka na kumwandama japokuwa katoka kula. Baada ya mafanikio yao akinamama hao walikuwa hawaishi kusema kwamba kujiendeleza ni uamuzi wa mtu na wala siyo muujiza au kipaji kama wadhaniavyo wengine. Maarifa waliyoyapata waliyatumia kwa utunzaji bora wa nyumba, afya za watoto, kilimo cha bustani, miradi ya uchumi na kadhalika.

Kwa upande wa Mpepo, alipenda michezo ya kunyoosha viungo - hasa mchezo wa kuruka kichura, kukimbia, mieleka na mingine kama hiyo. Alipenda michezo ya kutoa jasho. Kinyume chake hakupenda mchezo wa karata, bao na mingine inaayofanana na hiyo. Aliita michezo hiyo ni ya uvivu ingawaje alipenda burudani! Wakati mwinginw michezo hiyo ilimchukua nusu saa hadi saa moja na kuacha baada ya kutokwa na jasho la kutosha.

Wakati wote alipokuwa akishughulika na shughuli za kijiji, shamba lake lilikuwa linazidi kuongezeka na kustawi. Hakuna wakati alipolegeza jitihada zake maana alikwisha apa. Kajirekebisha na kawa na msimamo mpya tofauti na maisha duni na mikasa iliyoambatana na ujinga aliokuwa nao siku za nyuma.

Katika sura ifuatayo tunaona jitihada zake zinazaa matunda ambayo daima hasingeweza kuyapata. Matunda hayo ni pamoja na kuwa mtu mashuhuri, kiongozi hodari, mtu mwenye maisha bora na familia ya kupendeza.

## SURA YA NNE
### Matunda ya Jitihada

Hadithi ya Mpepo siyo ya pekee sana kuhusu maisha. Wako watu wengine ambao wamewahi kupatwa na misukosuko mingi huko nyuma kabla ya kuwa na maisha mazuri. Tofauti ni kwamba sio watu wote wamepata fursa ya kuweza kueleza maisha yao katika maandishi. Kadhalika kupata mtu au watu wenye shauku na ari ya kueleza historia ya mtu sio jambo rahisi. Kwa nadra sana watu mashuhuri; kama vile viongozi wa dini, viongozi wa kitaifa na kimataifa hupata fursa ya kuelezewa maisha yao kuanzia kuzaliwa, ujana au usichana wao na mafanikio na matatizo waliyopata. Jambo la kushangaza na la kweli ni kwamba mara nyingi maelezo hutolewa wakati muhusika au wahusika wamekwisha fariki. Hapo hupewa sifa nyingi ziwe za ukatili au za huruma na busara aliyokuwa nayo wakati wa uhai.

Hata hivyo wapo watu wachache ambao historia zao zimesimuliwa kabla hawajafa; mathalani Adolf Hitler, Idd Amin na baadhi ya wakuu wa nchi ambao maisha yao husimuliwa wakiwa na wadhifa wao. Ukweli mwingine ni kwamba wahusika wanapoona na kusoma historia zao huwa wanafurahi, lakini siyo Mpepo! Yeye hataki kabisa kusikia ugonvi baina yake na mfugaji Selemani. Aidha anachukia sana kukumbushwa dharuba iliyomkuta kule Tunduma, vilevile adha aliyokuwa akiipata kutoka kwa marafiki zake walevi.

Mpepo anakiri kwamba nguvu ambazo alizipoteza kule Tunduma na rafiki yake Luzolo, zingeweza kutosheleza kuolima shamba lisilopungua ekari sita na kuweza kulisha zaidi ya familia kumi likiwa limetunzwa vizuri. Hataki kusikia upuuzi ule tena! Shughuli za Mpepo zilizidi kupanuka hasa zile zilizomhusu yeye binfsi na familia yake…. ***Itaendelea...***

# ELIMU JAMII

## SAFARI YA MALEZI - 03

**MALEZI YA KUEPUKA**

**2.0 Malezi Sumu (Poisonous Parenting)**
Malezi sumu ni aina ya malezi yanayodhoofisha ukuaji wa mtoto kwa njia za kihisia, kiakili, na kijamii. Mzazi hageuki tena kuwa mlezi wa kweli bali anakuwa kama mwelekezaji wa maisha ya mtoto kwa mujibu wa ndoto, hofu, au matarajio yake binafsi. Matokeo yake, mtoto hukosa nafasi ya kuwa yeye mwenyewe. Hapa chini ni baadhi ya mitindo ya malezi sumu inayoonekana sana katika maisha ya Watanzania:

**2.1 Mzazi wa kuakisi ndoto za mtoto (mirror-image parenting)**
Mzazi huyu humchukulia mtoto kama kioo cha ndoto zake zilizoshindikana. Anamtumia mtoto wake kutimiza yale ambayo yeye hakuyapata maishani. Kwa mfano, mzazi ambaye alitamani kuwa daktari lakini hakufanikiwa, humlazimisha mtoto wake kuchukua mwelekeo huo bila kujali mapenzi au vipawa vya mtoto.
Hali hii pia hujitokeza pale ambapo mzazi anataka mtoto awe kama yeye – kama yeye ni mwalimu, basi na mtoto awe mwalimu; kama yeye ni daktari, basi na mto awe hivyo; yaani inafika wakatoi mzazi anaacha kumuhimiza mtoto wake afanye kwaa bidii, kwa kumpa ahadi ya kumwachia urithi, aje aiongoze maradi ya mzazi wake hapo baadae, sio jambo baya, lakini kama si chaguo la mtoto, anaweza kuja kukuhuzunisha sana hapo baadae.
Huu ni mzigo mzito kwa mtoto kwani haishi maisha yake bali maisha ya mzazi. Mwishowe, huibuka na chuki ya ndani au kukosa furaha kabisa maishani.

Imeandikwa na: Kelvin John Kyara: 0753767930

**2.2 Mzazi anayetafuta Utukufu Kupitia Mtoto (Shobik Parenting)**
Huyu ni mzazi anayemkuza mtoto kwa nia ya kujipatia sifa au hadhi ya kijamii. Humweka mtoto mbele ya watu kwa lengo la kusifiwa – kama kushinda mashindano, kuwa bora darasani au kuonekana na watu mashuhuri. Lakini ndani ya nyumba, mtoto huyu hupata mateso au kutokujali kihisia.
Kwa mfano, mzazi anaweza kujisifia kwamba mwanawe yuko shule ya kimataifa au anaimba kanisani vizuri, lakini hatilii maanani hisia au matatizo ya mtoto huyo. Mtoto hufanywa kuwa kioo cha nje cha familia lakini ndani ya moyo wake, hana furaha.

**2.3 Mzazi mwenye dhihaka au udhalilishaji (dismissive/derogative parenting)**
Mzazi wa aina hii hudharau au kudhalilisha mtoto mara kwa mara. Maneno kama "Wewe huwezi kitu", "*Mbona huwezi kama kaka yako?*", au "*Wewe ni mzigo tu*" huacha majeraha ya maisha.
Mtoto hukua akijiona si wa maana, hana thamani, na huanza kujiwekea mipaka hata katika ndoto zake. Katika familia nyingi, hali hii hujificha ndani ya maneno ya kawaida ambayo huonekana kama utani, lakini moyoni mtoto huumia.

**2.4 Mzazi mwenye mipango ya siri na udhibiti mkubwa (conspinous parenting)**
Huyu ni mzazi ambaye anataka kujua kila jambo kuhusu mtoto wake, hata yale ambayo si ya lazima. Anakagua simu, anadhibiti marafiki, huamua aina ya nguo, chakula, na hata saa za kulala – bila mazungumzo ya kuelewana.
Mzazi huyu anaamini kuwa "anamlinda mtoto", lakini kwa kweli anaharibu uwezo wa mtoto wa kujitegemea. Mtoto huyu hukua akiwa mwoga, asiyejiamini, au mwenye matatizo ya kijamii.

**2.5 Mzazi wa kumkinga kupita kiasi (mamoring/mamordad parenting)**
Mzazi wa aina hii humkinga mtoto hata katika mambo anayoweza kufanya mwenyewe. Hataki mtoto ashindwe, aumie, au ashindwe kukubalika. Kwa mfano, humzuia mtoto kucheza na watoto wengine kwa hofu ya kuumizwa au huingilia kila tatizo analokutana nalo shuleni. Hali hii humfanya mtoto kuwa mtegemezi, asiye na ustahimilivu wa kihisia, na asiyeweza kukabiliana na changamoto za maisha.

**2.6 Mzazi wa mapendeleo yasiyo ya kawaida (dearest parenting)**

Mzazi huyu humpenda mtoto fulani kuliko wengine, au humpa upendeleo wa pekee ambao hauendani na haki. Anaweza kumuita mtoto huyo "*kipenzi cha mama/baba*" na kumpa vitu au uhuru usiopatikana kwa watoto wengine.

Mapendeleo haya hujenga chuki kati ya watoto na kuharibu uhusiano wa kindugu. Hali hii huacha majeraha ya maisha si tu kwa wale waliopunjwa, bali hata kwa yule aliyetendewa vyema kupita kiasi.

***Tafakari***: Malezi haya sumu yamejificha sana ndani ya tamaduni, hofu, na matarajio ya wazazi wengi. Ni muhimu kwa mzazi kujitathmini: je, namlea mtoto kwa sababu ya hofu zangu au kwa sababu ya kumpa uhuru wa kuwa yeye mwenyewe? Mzazi mwenye hekima ni yule anayesimamia, si anayetawala;

**2.7 Malezi ya kudekeza: mtoto asiyeguswa**

Kuna wazazi ambao kwa mapenzi yao kwa mtoto ya kupitiliza, huamua kumpa mtoto kila anachotaka – awe mdogo au mkubwa. Mtoto hapaswi kukasirika, hapaswi kunyimwa, hapaswi kuguswa. Akilia anapewa, akisema hapendi, anaachwa, akitaka kitu chochote, anapewa – hata kama hakifai. Wazazi hawa huamini kuwa "kumpa kila kitu" ni njia ya kuonyesha upendo, lakini ukweli ni kwamba hii ni njia ya kuharibu maisha ya mtoto kimyakimya.

Mfano kuna sehemu moja nilikwenda mtoto wa miaka mitano, hawezi kula chakula bilaya kuwepo kwa kinywaji pembeni huku analishwa nab ado anaangalia piacha za vichekesho (katuni) kwenye simu aliyozawadiwa na wazazi wake.

Mtoto anayekuzwa kwa kupewa kila kitu bila kuwajibika, huwa mvivu, mwenye kiburi, asiye na huruma, na asiyejua kupambana na maisha. Hawezi kuvumilia changamoto wala kukubali kusahihishwa.

**Mfano halisi niliokutana nao:** Nilikutana na mwanafunzi mmoja wa shule ya sekondari ya bweni (high school), mvulana. Alikuwa hawezi hata kutandika kitanda chake, hajui kufua hata nguo zake ya ndani. Alikuwa amezoea kufanyiwa kila kitu nyumbani: mama anampikia, dada wa kazi anamfulia, mwingine anatandika kitanda chake, yaani alikuwa mvivu hadi wa kula chakula, alikuja akiwa bonge lakini wiki tu amepungua sana. Alipofika shule ya bweni, aliishi kama mgeni katika maisha ya kawaida. Alikuwa mnyonge, mwenye aibu, asiyejiamini, na wakati mwingine alikuwa analia kwa sababu ya kazi ndogo ndogo tu.

Mtoto kama huyu akiwa ni wa kike anapofikia hatua ya kuolewa au kuanzisha familia, anakuwa mzigo kwa mwenzake. Hebu fikiria binti huyu anapokwenda kwa mume – anatarajiwa apike hata mara moja kwa wiki, afue, apange nyumba… lakini hawezi. Hapo ndipo ndoa zinapoyumba kwa sababu ya malezi yaliyomharibu.

**2.8 Malezi ya kifalme**

Kuna aina ya malezi ambayo yanamfanya mtoto aishi kama yupo kwenye kasri la kifalme. Mzazi hupanga kila kitu – kuamka, kula, kulala, hata wakati wa kucheza – yote kwa ratiba kali kama ya jeshi. Mtoto hawezi kula chakula chochote kama hakipo kwenye ratiba au kama hakijapikwa kwa namna anavyozoea. Mbaya zaidi, kuna watoto hawawezi kula bila soda au juisi pembeni. Hawawezi kunywa maji ya kawaida.

Mtoto wa aina hii akifika sehemu yenye maisha tofauti – kama shule ya bweni, safari ya kijamii, au hata maisha ya ndoa – anakuwa kama amepotea. Anaishi kwa mazoea ya kifahari ambayo hayatambui uhalisia wa maisha ya kila siku.

Kuna wazazi pia hawaruhusu mtoto kujaribu ladha mpya. Mtoto anaambiwa, "Usile chakula hicho, si cha hadhi yako." Au analelewa kwa chakula maalum cha dukani – fast food kila siku, c*hips, burger, pizza*, nk akidhani ndicho bora. Lakini mwili unakosa virutubisho halisi, afya inaharibika kimya kimya, na tabia ya kuchagua-chagua huota mizizi.



## HAPPY NEW YEAR '08'—Twahir Yusuph

***Ilipoishia…***

**"Pole sana mkuu, kama nimeuliza swali ambalo halijakufanya ujisikie vizuri." "Najua upo kwenye misheni ngumu, na unastahili kuuliza chochote sasa kuhusu yeye. Hivyo ondoa shaka inspekta" "Nashkuru mkuu, ila ningependa kufahamu kitu kingine, hivi siku ya tukio uliwasiliana naye Imraan? Pia mbona yeye hakuwepo kwenye msiba wa rafiki yake?" aliuliza Inspekta.**

***Endelea...***

"Usiku baada ya tukio lile la kifo cha Jax, Imraan hakuwa sawa. Alilia kiasi hadi kufikia hatua ya kupoteza fahamu na kuzimia. Ilibidi tumpatie huduma ya kwanza na kumpumzisha. Asubuhi sisi kama familia tulitangulia tukimwacha, alisema angempigia simu Labi Kimati na kufika naye msibani, huyo ni rafiki yake pia, ambao wote pamoja ni rafiki yao na Jax."

Jina la Labi Kimati linatajwa kwa mara ya tatu masikioni mwake, mara hii inasadikika tena kuwa angepigiwa simu na Imraan ili waongozane wote hadi msibani. Ni asubuhi hiyo pia ya tukio la kifo cha Imraan. Ikawa taarifa nyingine hiyo iliyozidi kumsisimua Inspekta Kasese. Kwanini kila pahala Labi Kimati awepo? Akiwa kwenye udadisi Inspekta, CDF Rashidi Koboko akaendelea,

"...nilishtuka sana baada ya ile video iliyomuonesha Imraan akiwa kwenye mikono ya muuaji siku ile ya msiba, niliangaza mboni zangu kila pahala na kweli sikumuona, ila rafiki yake Labi Kimati alikuwepo." Akaweka tuo akimtazama Inspekta Kasese aliye makini kumsikiliza, kisha akaendelea, "sikupata hata muda wa kumuuliza ilikuwaje, akili yangu ilikuwa mbali, nadhani kila mtu aliyeshuhudia unyama ule alifahamu nilijihisi vipi nikiwa kama Baba.

Baada ya kila kitu kutamatika, tukiwa nyumbani kwangu, nilimuuliza Labi kuwa aliwasiliana na Imraan asubuhi ile?" Akaweka tena tuo, viganja vya mkono wake wa kulia vilikifuata kikombe cha kahawa kilicho juu ya meza waliyoizunguka. Akakinyanyua na kupiga funda mbili kisha akakirejesha. Inspekta Kasese ni kama alikuwa anaomba CDF Rashidi Koboko anywe haraka ili waendelee na mazungumzo yao, alipoishia ndipo pana jibu analolitaka. "Alikubali Labi, alisaili kuwa Imraan alimpigia na walipanga waje wote kwenye msiba ule wa rafiki yao, akanambia walikubaliana wakutane njiani na wangetumia usafiri wa Imraan. Lakini..." kabla hajamalizia kikohozi kilimpalia CDF Rashidi Koboko.

### 8

Alikohoa kisha akaendelea, "Labi alichukua *Uber* hadi walipopanga kukutana, lakini muda mfupi baada yeye kufika, akiwa anamsubiri Imraan, iliingia jumbe kwenye simu yake kupitia namba ya Imraan ikimtaka atangulie kuwa yeye atachelewa. Labi akamwambia Imraan kuwa atamsubiri hadi muda huo ili waongozane, lakini alikataliwa na kuambiwa tu awahi. Hakuwa na jinsi ilibidi afanye kama alivyotaka rafiki yake."

"Ulimwamini?" Inspekta Kasese aliuliza.
"Sio sana, hadi aliponionesha jumbe walizokuwa wakitumiana, na nilipozifanyia uchunguzi, baada ya hapo nilimwamini na kuridhia." CDF Rashidi Koboko alijibu huku akipiga funda lingine la kahawa. Kimya kikaishika midomo ya Inspekta, mboni zilionesha kudadisi kitu fikrani.

"Asante sana mkuu, nimefurahia maongezi haya, mi nadhani nimetosheka sasa." hakuwa na swali zaidi Inspekta Kasese.
"Nashkuru sana kwa kunitembelea pahala hapa, na nakukaribisha tena Inspekta, mimi nikutakie kila la kheri."
"Asante sana mkuu, pia nashkuru kwa kahawa." alijibu huku akinyanyua bilauri ndogo iliyo na kimiminika hicho, akapiga funda kadhaa kisha akaomba ruhusa ili aweze kwenda kuendelea na majukumu mengine.

* * *

Kama upendo ungelikuwa Bahari, basi huu ndiyo muda waliokuwa wanauogelea kwa kila mtindo walioutaka, kisha kupumzika kwenye fukwe zake wakiutazama na kuendelea kuburudika. Bila uongo, wawili hao waliishi upande ulio na kila aina ya kicheko cha kuyafurahia

mapenzi, kila dakika kwao ilibeba maana, pengine walikuwa kwenye kipindi cha juu kabisa cha mapenzi yao, yenye ladha ambayo hawakutamani siku waamke na wasiikute.

Huba lilijimwaya mno na kutaradadi kwa wachumba hao wawili, waliokuwa wanazisubiri siku chache ili waifunge ndoa itakayowapa kitanda halali kwa kila tendo la mahaba watakalolifanya. Mitoko ya sehemu za starehe na yoyote ambayo ingewapa tabasamu ilisheheni. Panapokucha, hadi muda kiza kinapolifukuza jua na kujipamba kwa mbalamwezi na nyota kadhaa angani, ndipo walipoihitimisha na kurudishana wanapoishi, hawakulala pamoja. Baada ya mizunguko mingi ya furaha tangu mchana wakiwa wote, muda huu walikuwa pamoja pia wakitembea barabarani.

Ni katikati ya jiji, ndani ya mitaa iliyotulia usiku huo, nyumba nyingi za hadhi zilijipanga kwa ramani, hakukuwa uswahilini. Ni wao tu wawili, viganjani walibeba Ice cream kila mmoja, wakiendelea kuzitupa nyayo zao taratibu huku vinywa vyao vikisemezana.

"Honey, napenda mno hii mitaa ilivyotulia hivi, huwa naburudika sana." sauti laini ya Vivi ilipenya masikioni mwa Labi, tena bila ghasia sababu ya utulivu uliokuwepo sehemu hiyo.


"Nimekumbuka siku tuliyokuwa tunatembea hivi tukikurudisha wewe baada ya kutoka klabu, Mimi, Jax, Imraan pamoja na wapenzi wao. Zilikuwa nyakati nzuri mno." ni maneno yaliyozifanya mboni za Vivi kumtazama Labi wake usoni, sababu yalimtoka kinywani kwa sauti ya kihisia mno.
Licha ya mizurulo mingi ya furaha, bado alionesha kuendelea kuwakumbuka rafiki zake hao ambao hawapo tena ulimwenguni. Vivi alielewa.

"Babe" aliita Vivi, "Hebu angalia kule." aliongea huku akionesha kidole pembeni, ubavu aliokuwepo yeye.
"Wapi?" Labi aliuliza akigeuza shingo yake, lakini ghafla alikumbana na Ice Cream ya uso. Vivi alimpakaza Labi Ice cream usoni na kuanza kukimbia, naye akawa anamkimbiza. Ukisikia mahaba ndiyo haya sasa. Mwanamke alizielewa hisia za mpenzi wake, naye hakutaka zijihisi unyonge ilhali yeye yupo karibu, alifanya kitendo hicho ili kumrejesha katika hali ya uchangamfu. Kilifanikiwa. Mbio zake zilibeba kingo fupi mno, Labi alimkamata Vivi na kuanza kumpakaza ya kwake pia huku wakifurahia.

Walikuwa hatua kadhaa mbele ya geti kubwa la nyumba yenye hadhi na muonekano mzuri. Katikati ya michezo yao ya kimahaba, hisia zikautaka mchezo mwingine uchezwe barabarani hapo. Ilitokea tu mkono mmoja wa Labi ukakizingira kiuno laini cha mrembo wake huyo, mwingine ukaambaa shavuni akimpapasa taratibu kwa hisia. Wote sura zao zilichafuka kwa Ice cream walizopakazana.

Afanye nini Vivi, pengine alisali kisirisiri Labi wake asiache kumfanyia hayo. Alitulia tuli akiusikilizia utamu wa mikono ya mpenzi wake iliyoendelea kuambaa juu ya ngozi yake teke huku sura zao zikiujenga ukaribu uliozifanya hadi pua zao kugusana.

“Vivi!” Labi aliita. Hiyo nguvu ya kutoa sauti kinywani ili aitike alikuwa nayo sasa? Ni pumzi tu za Vivi zilizosikika bila mpangilio, ndizo zilizotoa ishara kuwa amesikia ila kujibu hawezi. Akiwa kileleni mwa hisia za juu kabisa zilizompa uziwi na upofu kwa sekunde hizo chache, Vivi alihisi kucheleweshwa, au pengine kule kuitwa jina lake kulimfikia na ujumbe wa anachopaswa kukifanya ambacho alishakifahamu. Juu juu kama anayeishiwa pumzi, taratibu alikuwa akiipeleka midomo yake kuifuata ya Labi iliyowazi pia. Aliipata, akaganda hapo akiipa ambacho hisia zake ilikitaka kutoka kwa mpenzi wake huyo wanayependana. Sekunde chache mbele, ile midomo yao iliyonasana na kupasiana ndimi zao zilizogalagazana kinywani, iliacha.




***Itaendelea...***

# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (03)- Na: Eva Mrema

**Ilipoishia..**

**Miso aliondoka na kutuacha peke yetu. Sunche alinyanyuka kijasiri japo maumivu yalikuwa dhahiri shahiri; akanikaribia, akanitazama weeh! "*Can I hug you Tabita?* Akaniuliza. Nilihisi raha hadi kwenye unywele wa mwisho.**
**Nililitoa koti na kulisalisha kitini. Nilimkumbatia kwa nguvu hali nikijitahadharisha juu ya mkono wake wenye kidonda.**

***Endelea…***

Mara hii ni kama kila mmoja alijipumzisha mwilini kwa mwenzake. Tuliegemeana. Sikuweza kuuhesabu muda maana sikutamani uishe.
Sikumbuki kama nimewahi kumiliki amani kama hii mikononi mwa mwanaume. Nilijitoa kwenye kumbatio baada ya kuhisi mfumo wote wa mwili wangu unababaika. Tulianza kutazamana kwa ukaribu sana. Alinizidi urefu kidogo maana mimi pia si haba, nina kajiurefu fulani ka kuniruhusu kushiriki kwenye shindano lolote la ulimbwende duniani. Yeye sasa, ni mfano wa mwanaume kwenye ndoto ya kila mwanamke linapokuja swala la mapenzi.

Macho yaliunganisha waya uliopeleka mawasiliano moyoni, moyo ukaweka bayana matamanio yake, midomo ikaanza kukaribiana, ilikuwa hisia ya kipekee, kwa mara ya kwanza nilijiambia filamu za 'ki-hindi' haziongopi. Imekuwaje kwani? Nazamaje penzini kibubu namna hii? Mwanaume hajawahi hata kunichombeza, mkonyezo kidogo tu nishajirahisisha? Hapana kwa kweli, hapana Tabita," nilipitisha mkono katikati ya midomo yetu na wote tukagutuka.

Tulicheka na kutakana radhi. Niliketi na Sunche alilala kitandani. Dakika chache, mlango ukagongwa na sote tukatolewa kwenye uzingativu wa kutazamana ki wiziwizi. Aliingia Miso.

"Bosi nimekuletea sharubati, naomba kama utaridhia niende nyumbani, mke wangu kapiga simu mtoto ana homa, nitaelewa kama itanilazimu kubaki," Miso aliongea kwa unyenyekevu. "Niko sawa, nenda" Sunche alijibu. Miso akashukuru na kutoka ndani ya chumba kile binafsi cha hospitali. Miso alipishana na muuguzi aliyepita kuwataka wagonjwa wapumzike. Alitusabahi mrembo yule na kusihi sana mgonjwa alale mapema, kisha akaondoka zake. "Naomba niende nikuache upumzike bila shaka umesikia asemayo muuguzi." Nilimwambia. "Naomba ubaki na mimi, tuna mengi ya kusemezana, sina mpango wa kulala sasa hivi." Aliongea Sunche.

Tulianza kwa ukimya, kisha Sunche akafungua mazungumzo kwa hadithi nzuri kumhusu marehemu mama yake. Nilifurahia na nilisononeka wakati huohuo. Ni kama kila aliyempoteza mama yake ana mengi ya kusimulia kumuhusu. Shauku yangu ni kusikia kitu tofauti na hadithi za watu wengine. Nilitamani aiongelee hadithi yangu na yeye kwenye kurasa zijazo za kitabu kizuri cha maisha yake. Nilitaka tu aanze na neno "nilipokuona kwa mara ya kwanza" na atamatishe na "nataka uwe mwanamke wangu" Kila alipofungua kinywa moyo ulitabasamu kwa kuhisi muda umewadia hakika haikuwa hivyo. Matarajio yalinifanya nijione mnyonge sana. Matarajio yalinifanya nimuite domo zege na nimkejeli kwa maneno mengi ya kuchukiza. Sikuwa na ujasiri wa kuweka mawazo yangu bayana. Niliumilia ndani kwa ndani tu


**RIWAYA: NGUVU YA KIAPO**

Inapatikana katika kitabu (nakala ngumu) na soft copy (nakala tepe) kwa bei ya kirafiki.

**KITABU** - Tsh 10,000
**Dar es salaam:**
- Duka la Kona ya Riwaya - 0655428085
- Kalamu Tulivu Magomeni - 0718975659
- Posta Mpya kwa Joji - 0713454152
- Temeke kwa Eva Mrema - 0742630141

Soft Copy (Nakala tepe) PDF - Tsh 5,000
'Offer' kupitia Ngurumo ya Mwandishi ni - Tsh 3,000
Lipa kwa **MPESA LIPA NAMBA 36499709 Eva John Mrema**


## SURA YA TATU.

Jukumu la kumuuguza Sunche nililivaa na visa vingi ndani yake. Nilijidekeza na kumkumbatia bila sababu ili

# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (03) - Na: Eva Mrema

hatimaye afunguke. Nilidiriki kumuita rafiki hali moyoni nikijiambia yeye ndo chaguo la nafsi yangu. Baada ya siku nne kidonda chake kilipata unafuu. Aliruhusiwa kwenda nyumbani huku akipewa dawa kibao za kumeza. Alitakiwa kutazamwa na mtaalamu mara kwa mara ili kidonda chake kisipate maambukizi. Kilitakiwa kifanyiwe usafi kila ilipohitajika. Alitakiwa kliniki kila baada ya siku tatu. Maelezo yote ya dakitari tuliyasikiliza kwa pamoja. Msaidizi wake hakuwa kafika. Nililazimika kutumia gari langu kumsindikiza nyumbani kwake. Alinipa maelekezo ya njia isiyo na msongamano. Niliendesha kwa umakini, na kwa hakika alisifia udereva wangu. Tuliingia ndani ya mjengo baada ya kufunguliwa geti. Alinielekeza pa kuegesha, nami nikatii. Nilishuka na kwenda kumpa msaada wa kushuka garini. Ni kama alinidekea hivii, ila mimi sikujali wala nini.

Nilimfaa kwa dhiki kama rafiki, japo kamoyo kalinipwitapwita balaa.
Tuliingia ndani ya nyumba alimoishi. Palipangwa, pakapangika. Ndani ni kusafi haswaa! Na ukuta ulikuwa mtupu kabisa. Hakukua na picha, jambo lisilo la kawaida kwa wazungu. Usiulize nimejulia wapi. Ukiangalia sinema zao, umewahi ona Mzungu hana picha ya familia ama watu anaowajali? Kanishangaza. Nilihifadhi vitu vyake tulivyotoka navyo hospitali, kisha nikaaga kuondoka. Alinisihi sana nimsaidie akoge. Hapa jaribu limempata wa kumjaribu. Yaani mimi na jaribu langu tulipimana ubavu waziwazi.

Nilichukua kichemshio cha umeme, muonekano wake ni kama kichuma kilichojinyongorota mithili ya utumbo. nilikitia kwenye ndoo yenye maji na kukiwasha. Nilirejea sebuleni ili nimtaarifu akapunguze nguo ila sikumkuta. Niliita mara mbili ndipo akaitika. Sauti ilitoka upande wa pili wa nyumba nami nikaifuata. Niliviacha nyuma vyumba viwili na nilipofika cha tatu kilikuwa wazi. Niliingia kama ujumbe mfupi wa maneno. Nilimkuta akijitahidi kutoa fulana yake mwilini nikamsaidia. Akavua na suruali kisha akaniomba taulo lake alilolitundika sehemu maalumu ya kuhifadhia taulo ndani ya bafu lake. Nilimletea, papo hapo nilielekea nilipoweka maji. Tayari yalichemka. Nilizima umeme na kurejesha kichemshio mahali pake. Niliyabeba maji na kumpelekea.

Nilikuta tayari kaingia bafuni. Nilimhabarisha uwepo wangu naye akanitaka nimpelekee maji ndani.

Niliingia bafuni. Maji niliyapooza na kisha nilimuuza nawezaje kumpa msaada wa kukoga. Alinielekeza na mimi bila ajizi nilimfaa sana. Nilitoka bafuni, moja kwa moja niliondoka. Sikuaga wala kujieleza, niliondoka. Kwakuwa tayari nilikuwa karibu naye kwa siku kadhaa, nilimiliki mawasiliano yake na ya msaidizi wake, Miso. Nilimtumia ujumbe Miso na kumtaka afike haraka. Niliwasha *ndinga* yangu na kuondoka. Ilikuwa jumatatu, kwa muda niliorejea, nyumbani mdogo 'angu alitamalaki, sikutaka anione katika hali ile. Nilipitia kwenye bustani ya umma. Nilikaa ili nijitulize. Nilijiuliza maswali yaliyokosa kabisa majibu ya uhakika.

*Nimekuwaje kwani? Hisia hizi nimezitoa wapi Tabita mimi? Mbona kama ni pepo limenivagaa, kuwa karibu na Sunche kwangu ni zaidi ya mateso matamu. Nifanye nini mimi mtoto yatima?* Kumbukumbu za muda mfupi uliopita zilinijia, za namna Sunche alivyokuwa akinitazama kwa karibu tukiwa bafuni, alinisogelea kihisia na kuniuliza maswali ya kawaida sana, kichokozi. Ni kama alikuwa akinitega hivii!

Binafsi nilijiambia mara nyingi, hiyo ndo namna yake ya kuonesha mapenzi, lakini akili ikakataa. Nikasema ama ndo wazungu walivyo ukija kwenye swala la kuonesha mapenzi, ila bado utamaduni wangu ukanikaba.

"Hakuna raha kama kutongozwa na mtu ambaye moyoni mwako amejaa. We muulize mwanamke yeyote aliye mapenzini atakuthibitishia hili. Naogopa kuonekana bidhaa rahisi, ama sivyo ningemwambia anitongoze, au ningemtongoza mimi yaishe".

Nilitafakari kwa kina na kujifariji. Nilikumbuka sekeseke nililolipitia kwenye husiano langu lililopita nikatabasamu tu.

"Tatizo napenda vibaya Tabita mimi" Nilijivuta kivivu na kurejea nyumbani. Niliitamatisha ratiba ya siku hiyo na mdogo wangu. Tulipika na kula pamoja, baada ya hapo kila mtu aliaga kwenda kulala. Sijui kuhusu mdogo 'angu, binafsi usiku uligeuka mrefu kuliko barabara iendayo nisipopajua.

***Itaendelea...***

## Tangazo

*Tangaza nasi kwa tsh 5000 tu*

*Hapa!*

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi
jamvilasimulizi@gmail.com